Stanbic Bank

TOLEO LA 5

# BAROMETA YA BIASHARA YA AFRIKA

MUONEKANO WA SASA WA BIASHARA YA MIPAKANI AFRIKA



TANZANIA

# DIBAJI

Siku zote biashara imekuwa nyenzo muhimu ya maendeleo ya Afrika, lakini kwa muda mrefu sana wale waliotaka kuelewa, kusaidia na kuikwamua biashara ya Afrika imebidi wategemee taarifa kidogo ya zamani au iliyotayarishwa nje. Kihistoria data kidogo iliyokuwepo iliandaliwa kwa kiasi kikubwa na asasi za kimataifa kama Umoja wa Mataifa, Benki ya Dunia na Shirika la Fedha la Dunia, nzuri lakini aghalabu hucheleweshwa -wakati ambapo maoni mengine yaliathiriwa na uzoefu wa mashirika makubwa ya kimataifa ambayo uhalisia wake unatofautiana sana na biashara ndogo na za kati za Kiafrika.

Ili kushughulikia pengo hili tulianzisha Barometeta ya Biashara ya Afrika ya Standard Bank-kielezo cha msingi kilichojengwa kutoa taarifa mpya inayotegemewa ya Afrika kuhusu mazingira halisi ambayo biashara hufanyika kwenye bara hilo. Barometa imetayarishwa kuwawezesha wajasiriamali, mashirika, wawekezaji, watungasera na wanataaluma kupata taarifa wanayohitaji kukabiliana na vikwazo vya biashara na kugundua fursa kwa ukuaji.
Barometa inashughulikia masoko muhimu 10 ya Kiafrika: Angola, Ghana, Kenya, Msumbiji, Namibia, Nigeria, Afrika Kusini, Tanzania, Uganda na Zambia. Kwa pamoja uchumi wa nchi hizi umewakilisha 57% ya GPD ya Nusu ya Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara. Mkusanyiko huu wa shughuli za kiuchumi unaonyesha umuhimu wa masoko haya na athari ambayo kwa pamoja zinaweka kwenye mwelekeo wa biashara ya Afrika.

Kadiri tunavyoingia mwaka 2026 dunia inajikuta katika mabadiliko. Utaratibu wa ushuru wa utawala mpya wa US umesababisha kukosekana kwa utulivu mkubwa na urekebishaji mpya katika mtiririko wa biashara ya dunia. Ushuru wa uagizaji wa juu katika sekta muhimu, shinikizo jipya katika ushirika wa kisiasa wa kanda, na sera jadidi za utaifa zimeongeza kipindi ambacho sasa kinaweza kuelezwa kama utaratibu mpya wa dunia.

Tunaishi katika kipindi chenye dhoruba na kutotabirika-lakini pia chenye fursa nyingi. Kwa Afrika, bara ambalo kihistoria lilitengwa katika mfumo wa zamani wa dunia, usumbufu huu unatoa mwanya adimu wa kujipanga upya. Mchanganyiko wa mpango mpya wa seradunia, mabadiliko ya utaratibu wa ugavi na mahitaji ya masoko mapya inatoa nafasi kwa nchi za Kiafrika kushika nafasi muhimu zaidi katika biashara ya dunia. Kutokana na msingi wa mteja wetu tayari tunaona athari halisi za mabadiliko haya. Biashara nyingi zinageukia Standard Bank kwa msaada katika kutafuta wasambazaji wapya, kubadilisha masoko mapya na kuongoza fursa mpya zinazosukumwa na ushuru. Hili liko wazi zaidi katika majadiliano yetu ya ukanda wa biashara Afrika-China. Ufumbuzi wetu wa uagizaji wa China na Afrika unaendelea kuwasaidia watengezaji wa Kiafrika na wachakataji mazao kupata vifaa na teknologia zenye ubora wa kidunia na uongezaji endelevu nchini China. Kinyume chake Mapendekezo yetu ya Uuzaji Nje ya Afrika na China- yaliyotolewa kupitia mtandao wetu mkubwa na ushirika wa kimkakati na ICBS, benki kubwa kuliko zote China- yamesaidia wasafirishaji nje wengi wa Kiafrika kupata mikataba ambayo imebadilisha kimsingi muelekeo wa biashara zao.

Simulizi hizi zinaonyesha vyote, umuhimu na ahadi ya zama mpya: Afrika inaweza na sharti itimize wajibu mkubwa katika biashara ya dunia.

Afrika inapitia mabadiliko makubwa ya kiuchumi. Bidhaa nyingi za kilimo sasa zinachakatwa mapema, na kuongeza thamani ya usafirishaji nje pamoja na kusukuma ukuzaji wa viwanda na upatikanaji ajira katika jamii za vijijini na mijini. Mabadiliko haya yanatokea pamoja na ukuaji mkubwa wa miji, ambayo yanaongeza mahitaji ya miundombinu mipya, teknolojia endelevu na uwezo mpya wa viwanda ambavyo sehemu yake kubwa imetokana na biashara ya dunia.

Mabadiliko ya hali ya hewa yanaongeza haja ya nishati mbadala, teknologia ya maji na kilimo bora. Bidhaa inabaki kuwa mhimili wa kufungua suluhishi hizi na kuhakikisha uthabiti wa bara.

Wakati huohuo, hifadhi muhimu ya madini ya Afrika na haidrokaboni vinaiweka katika moyo wa mnyororo wa thamani wa dunia unaochipukia na fursa nyingi katika unufaikaji na uchakataji bora.

Umoja wa Kifedha kupitia Eneo la Biashara Huria la Bara la Afrika unaimarisha msingi kwa ajili ya soko la kiushindani zaidi na soko linalojitegemea Afrika. Ukichanganya na uchumi wa kidigitali ambao unakua kwa kasi-na kuwezesha biashara ya mtandaoni, huduma za kidigitali na ushirika mpana zaidi wa biashara ndogo-Afrika inaweka kazi ya msingi kwa ajili ya wimbi lijalo la ongezeko la biashara.

Msingi wa yote haya ni nguvukazi chanya na madhubuti ya Afrika ambayo inatoa moja ya faida kubwa zaidi ya wingi wa watu duniani. Utumiaji wa fursa hii utaimarisha uwezo wa uzalishaji wa bara, masoko ya ulaji na ushindani wa muda mrefu katika biashara ya dunia.

Wakati dunia inatafuta vyanzo vipya vya uthabiti na vituo vipya vya ukuaji, Afrika inasimama katika mwanzo wa uwezekano. Biashara itakuwa kiwezeshi muhimu cha mabadiliko haya- na ya kuaminika. Data maalumu ya Afrika itakuwa muhimu katika kusaidia biashara, serikali na wadau wa maendeleo kufanya uamuzi sahihi katika mazingira yasiyo na uhakika.

Barometa ya Biashara ya Afrika ya Standard Bank ni mchango wetu katika misheni hiyo: wajibu kwenye mwanga unaong'aa ambako taarifa ni adimu, kuwezesha vitendo pale ambapo awali kulikuwa na kusita, na kusaidia safari ya bara kuelekea kuwa mshirika mwenye athari kubwa katika biashara ya dunia.

Naamini toleo hili la Barometa litakupatia utambuzi, uwazi na mtazamo unaohitaji uongozaji wa fursa na changamoto za usoni.

## Philip Myburgh

**Mdhamini Mkuu**
Barometa ya Biashara ya Afrika ya Standard Bank
Mkuu wa Kitengo: Huduma za Kibenki za Biashara ya Kuuza na Kununua



# NYUMA YA BAROMETA

## Kuwezesha matokeo: Kuchochea mabadiliko

**Nyuma ya kila kielezo sahihi cha biashara sio tu kuna data lakini pia mpango, nidhamu na utekelezaji mzuri.** Hii ndiyo hadithi nyuma ya Barometa ya Biashara ya Afrika ya Benki ya Stanbic.

**Barometa ya Biashara ya Afrika ni zaidi ya chapisho.** Ni jukwaa la inteligensia ya mali lililojengwa kuimarisha uwelewa wa mienendo ya biashara katika nchi kumi za Afrika zenye masoko makubwa. Kutokana na mtazamo wa kimasoko na kiufundi wajibu wetu umekuwa kugeuza ishara za kiuchumi ngumu kuwa mitazamo ya kimkakati inayoweza kupatikana na kuhakikisha kwamba Barometa inatumika kama nyenzo ya kuaminika kwa benki, wateja wake, watunga sera na wasomi.

**Kimsingi Barometa inaunganisha aina mbalimbali za inteligensia.** Inajukumuisha data za kuaminika za kiuchumi mkuu na kifedha kutoka asasi kama Benki ya Dunia, Shirika la Fedha la Dunia, Kituo cha Biashara za Kimataifa, benki kuu za nchi na Kitengo cha Uchumi cha Benki ya Stanbic, pamoja na uchambuzi wa kiuchumi wa kitaalamu na mitazamo bora inayopatikana moja kwa moja kutoka kwa washirika wa masoko.

**Muhimu ni kwamba utafiti unakwenda zaidi ya viashiria vya kiuchumi ambavyo vipo.** Kutokana na utafiti mkubwa na mahojiano ya kina na wafanyabiashara, watoa uamuzi na wadau wa tasnia kwenye maeneo mbalimbali, Barometa inapata ukweli halisi wa biashara za ndani na mpakani. Kwa wastani takriban 65% ya biashara zilizopitiwa ni biashara ndogo, ili kuhakikisha kwamba maoni ya wale ambao wanafanya mhimili wa mfumo wa kibiashara wa Afrika wanawakilishwa vya kutosha.

**Kwa kuwahusisha wafanyabiashara katika maeneo ambayo shughuli za biashara** ni kubwa sana, utafiti unatoa hali halisi ya biashara, ikiakisi sio tu vipimo vya utendaji, lakini pia hisia, vikwazo na fursa.

Wajibu wetu umekuwa ni kuhakikisha kwamba inteligensia hii ni timilifu, sahihi na kuwakilishwa kimkakati, ili kutafsiri ugumu wa kiuchumi kuwa utambuzi ambao unasaidia uamuzi na kuimarisha uongozi wa Benki ya Stanbic katika kufanikisha biashara katika bara lote.

Barometa ya Biashara ya Afrika inasimama kama tafakuri ya azma hiyo: mtazamo wenye uadilifu, umuhimu na athari.


### Italia Matlala

**Mkuu wa Kitengo:** Chapa na Masoko
Standard Bank: Kitengo cha Wateja wa Biashara






# JEDWALI LA MAUDHUI


Muhtasari Mkuu

1 Utangulizi

2 Barometa ya Biashara ya Afrika ya Benki ya Stanbic Toleo la 5 Viwango vya Nchi.

3 Mazingira ya Uchumi Mkuu

4 Uimara wa Uchumi Mkuu

5 Msaada wa Serikali

6 Vikwazo vya Miundombinu na Wawezeshaji

7 Uwazi wa Biashara

8 Mwenendo wa Kifedha wa Wafanyabiashara na Upatikanaji wa Fedha

9 Biashara ya Nje na Ufanyaji Biashara Afrika

Hitimisho

Viambatisho

Kuhusu Utafiti

Katao


## NAMNA YA KUPITIA WARAKA HUU

**Bofya kwenye sehemu katika Jedwali la Maudhui ili kuitumia.**

Sura ya awali ya matumizi juu ya kila ukurasa inakusaidia kupitia haraka katika sehemu tofauti..

Bofya kitufe mama kurejea kwenye Jedwali la Maudhui.

Bofya kwenye kitufe cha mbele na nyuma kwenda kwenye ukurasa ufuataoau uliopita.

Skani kusoma Ripoti mtandaoni

# MUHATASARI MKUU

Ikiwa ni benki kubwa Afrika, Standard Bank (ikifanya biashara Tanzania kama Stanbic Bank) imeonyesha uwepo na ustadi wake katika bara lote na kufanya Barometa ya Biashara ya Afrika ya Benki ya Stanbic (SBATB).

FUNGUO ZA RIPOTI

▲ ▼ Mishale inaonyesha ongezeko/ Punguzo kubwa kitakwimu kutoka utafiti uliopita

SB ATB ilizinduliwa mwaka 2022 kwa madhumuni ya kuanzisha kielezo cha biashara kinachoongoza Afrika kuziba ombwe la taarifa za kuaminika kuhusu data ya biashara ya Afrika na kusaidia kuwezesha ukuaji wa biashara ndani ya Afrika. Upatikanaji wa data bado ni changamoto Afrika yote na SB ATB inakusudia kujaza sehemu ya ombwe hili la data kwa kupata mapitio ya data ya maoni ya biashara za Afrika kwenye mazingira ambayo itaendeshwa, tabia, shughuli na mitazamio yake.

Toleo hili ni la 5 la SB ATB. SB ATB inalenga nchi 10: Angola, Ghana, Kenya, Msumbiji, Namibia, Nigeria, Afrika Kusini, Tanzania, Uganda na Zambia.

Ili kutengeneza kielezo cha viwango vya SB ATB, aina saba za aina za data zinakusanywa kutoka vyanzo asilia na vya pili.

Aina hizi za kimantiki ni uwazi, upatikanaji pesa, uimara wa uchumi mkuu, miundombinu, biashara ya nje, utawala na uchumi na mwenendo wa kifedha wa wafanyabiashara. Hivi ni vipimo saba ambavyo alama za barometa kwa kila nchi vinatumika.

Kutoka mtazamo wa data ya msingi Mapitio ya Barometa ya Ubora wa Biashara ya Benki ya Stanbic yanatayarishwa.

Alama za SB STB na vipimo kwa nchi ni wastani wa data yote iliyokusanywa kutoka mapitio ya utafiti wa msingi yaliyofanywa kwa makampuni 2218 katika zile nchi kumi zilizochaguliwa.

SB ATB ni mkusanyiko wa SB QTB na SB STB.

Hii ni Ripoti ya Tanzania. Inakusanya uchambuzi wa data ya msingi na ya pili iliyokusanywa maalumu kwa Tanzania kati ya Septemba na Octoba 2025 inayoonyesha mienendo na fursa za biashara ndani ya nchi.

Nafasi ya jumla ya Tanzania katika kiwango cha SB ATB ilibaki nafasi ya 4 Agosti 2024 na katika msisitizo wa utafiti huu. kuhusiana na SB STB nafasi yake ya 7 haikubadilika. Aidha Tanzania ilishikilia nafasi yake ya 1 katika SB STB. Kwa hiyo utendaji wake usiobadilika katika SB QTB na SB STB ilifanya kubaki na nafasi yake ya jumla SB ATB kulingana na masoko mengine. Ni muhimu kujua kwamba nafasi ya SB ATB ya nchi nyingine inalinganishwa na nchi 10 zenyewe. Kwa maneno mengine nchi zinapangwa dhidi ya nyingine, yaani alama miongoni mwao.

**Tanzania ilibaki na nafasi ya 4 katika viwango vya jumla vya SB ATB kama vile Agosti 2024.**

Jedwali la hapa chini linaonyesha utendaji linganishi katika aina za kimakundi za SB ATB.

**Utendaji SB STB wa Kenya katika makundi saba**




**Angalizo:** Viashiria vyote (isipokuwa wepesi wa biashara) vina alama za kielezo kuanzia 0 hadi 100 ambapo 0 inawakilisha alama ya chini na 100 alama ya juu kabisa. Kwa wepesi wa kiashiria cha biashara: 0 inawakilisha alama ya juu na 100 alama ya chini.

Okt 2025
Aug 2024

Tanzania ilibaki nafasi ya 4 katika viwango vya Barometa ya Biashara ya Afrika ya Benki ya Stanbic na kupanda hadi nafasi ya 31 Oktoba 2025 kutoka nafasi ya 25 Agosti 2024.

Muonekano wa kiuchumi wa nchi umebaki mzuri kwa vile ukuaji wa GDP ulikadiriwa kuwa 5.9% mwaka 2025 na kutazamiwa kufika 6.4 mwaka 2026. Uthabiti huu unasaidiwa na kuchaguliwa tena kwa Rais Samia Suluhu Hassan Oktoba 2025 inayoonyesha mwenelezo wa sera na utulivu kwa jumuia ya biashara. Mfumuko wa bei ulibaki chini kwa wastani wa 3.4% mwaka 2025 wakati akiba ya fedha za kigeni ilibaki USD bilioni 6.65 hadi Septemba, 2025.

Kielezo cha ufanisi wa uimara wa biashara Tanzania kilikua kidogo hadi 73 Octoba 2025 kutoka 72 Agosti 2024. Hisa za mapitio ya biashara kuonyesha matumaini ya ufanisi wa uchumi ziliongezeka hadi 74% katika msisitizo huu, ikisukumwa kwa kiasi kikubwa na biashara ndogo. Maoni haya chanya yanafanana na upanuzi unaoendelea wa sekta ya viwanda, ambapo Kielezo cha Uzalishaji wa Viwanda kilikuwa 7% katika robo ya tatu ya mwaka 2025. Licha ya matumaini haya mapitio ya biashara yalionyesha tahadhari kuhusu athari za mapato kama 86% ya wasiwasi ulioelezwa kuhusu msinyao wa viwanda.

Kielelezo cha ufanisi wa msaada wa serikali kiliongezeka hadi 69 Octoba 2025 kutoka 65 Augusti 2024.

Mapitio ya biashara yaliona kuwa Serikali imekuwa na msaada mkubwa kwa biashara ya mpakani, wakati 61% ilikadiria vizuri katika msisitizo huu kulinganisha na 54% Augusti 2024. Mafanikio haya yanahusishwa na mabadiliko kama kuanzishwa kwa matayarisho ya Mpango wa Pili wa Usimamizi wa Marekebisho Aprili 2025 na uanzishwaji wa Mamlaka ya Kiuchumi Tanzania Julai, 2025. Zaidi ya hapo uanzishwaji wa Dawati la Taarifa za Biashara katika mpaka wa Taveta-Holili Octoba 2025 umesaidia kushughulikia vizuri vizuizi visivyo vya ushuru. Ubora wa kielezo cha ufanisi wa miundombinu na biashara Tanzania umeboreka hadi 68 Octoba 2025 kutoka 64 Agosti, 2024. Mapitio ya biashara yalionyesha ubora zaidi katika aina za miundombinu mingi, pamoja na usambazaji maji, uliopanda baada ya kukamilika kwa Mradi wa Maji na Usafi wa Mazingira wa Ziwa Victoria Juni, 2025. Viwango vya meli pia viliongezeka kiasi kikubwa baada ya kuanza kwa shughuli za usafirishaji za SGR kati ya Dar es Salaam na Dodoma Juni 2025. Kiwango cha ugavi wa umeme kiliongezeka kwa kuwa Mradi wa Umeme wa Julius Nyerere uliunganishwa kikamilifu katika gridi ya taifa Februari 2025.

Upatikanaji wa kielezo cha ufanisi wa mikopo kilipanda hadi 62 Octoba 2025 kutoka 59 Agosti, 2024.

Kiasi kikubwa cha mapitio ya biashara kiliona kwamba upatikanaji wa

mikopo ni rahisi katika msisitizo huu ambapo 51% wakitoa maoni chanya kulingana na 44% Agosti, 2024. Mabadiliko haya yanaimarishwa na Benki Kuu ya Tanzania kushusha Kiwango cha Riba Benki Kuu hadi 5.75% Octoba 2025 na utekelezaji wa Kampuni ya Dhamana ya Mikopo mwaka 2025 kusaidia MSME. Mapitio ya biashara ndogo kuonyesha ukosefu wa dhamana kama kikwazo yalishuka hadi 46% katika msisitizo huu kutoka 65% Agosti 2024.

Kiwango cha kielezo cha unafuu wa biashara Tanzania kiliongezeka hadi 48 Octoba 2025 kutoka 46 Agosti 2024.

Mapitio ya biashara yalionyesha ufanyaji biashara na dunia yote kuwa rahisi zaidi; na kupanda hadi 22% katika utafiti huu. Mabadiliko haya kwa kiasi fulani yametokana na China kutekeleza sera ya kutotoza ushuru wa forodha kwa mauzo ya nje kuanzia Desemba 1, 2024. Wakati kufanya biashara na washirika wa nje kumekuwa rahisi, biashara zilizopitiwa zimeelezea kuongezeka kwa upinzani kuhusu biashara na Afrika yote, wakati 53% waliona kuwa sio rahisi wala ngumu katika utafiti huu.

Kielezi cha kiwango cha uwazi wa biashara kimeongezeka hadi 58 Octoba 2025 kutoka 51 Agosti, 2024. Waagizaji waliohojiwa wanaongezeka kuagiza kutoka China katika utafiti huu kulingana na 43% Agosti, 2024. Hali hii inachochewa na miradi ya miundombinu kama SGR ya Tanzania-Burundi, iliyozinduliwa 2025 ambayo huhitaji mitambo mizito. Hata hivyo mauzo ya nje kwenda Afrika Mashariki yalikutana na changamoto kutokana na kanuni mpya mnamo Julai 2025 zilizowakataza wageni kufanya biashara ndogo na nyingine.

Tanzania imeonyesha uthabiti na kukuza mazingira ya biashara yakisaidiwa na mtazamo wa kiuchumi-mkuu na uwekezaji wa miundombinu ya kimkakati. Serikali inaendelea kukuza hali ya kiuchumi kupitia mageuzi ya udhibiti na uondoaji wa vikwazo vya biashara, wakati biashara zilizotafitiwa zinaonyesha ukuaji wa kujiamini katika uchumi. Ingawa mienendo ya biashara ya kikanda inatoa changamoto, nchi inafanikiwa kuimarisha uhusiano na masoko ya dunia, husussan Asia. Mtazamo endelevu kwenye upatikanaji mikopo na maendeleo ya miundombinu yumkini yataendeleza kasi chanya huko mbele.

.

## Muonekano wa kiuchumi wa nchi umebaki mzuri

**kwa kuwa ukuaji wa GDP ulikadiriwa kuwa 5.9% mwaka 2025 na kutegemewa kufikia 6.4% mwaka 2026.**

**Kiasi cha biashara zilizopitiwa ambacho kinaonyesha matumaini kuhusu utendaji wa nchi kiliongezeka hadi 74% katika**

## utafiti huu kwa kiasi kikubwa na biashara ndogo.

## Serikali inaendelea kukuza hali ya biashara kupitia mabadiliko ya udhibiti na uondoshaji

**wa vizuizi vya biashara wakati ambapo biashara zilizopitiwa zinaonyesha ukuaji wa kujiamini katika uchumi.**



# 1 UTANGULIZI

Ikiwa ni benki kubwa zaidi Afrika Standard Bank (ikifanya biashara Tanzania kama Stanbic Bank) imeonyesha uwepo na ustadi wake katika bara lote na kufanya Barometa ya Biashara ya Afrika

## Benki ya Stanbic (SB ATB).

SB ATB ilianzishwa kwa madhumuni ya kuunda kielezo cha biashara kikubwa Afrika kuondoa ombwe la data ya kuaminika ya biashara Afrika na kusaidia na kuwezesha ukuaji wa biashara baina ya nchi za Afrika.

Biashara-kwa muktadha wa SB ATB sharti ieleweke kama mchakato wa uzalishaji na uhawilishaji wa bidhaa na huduma ambazo unawezeshwa na suluhisho ambazo zinaunganisha vizuri mnyororo wa usambazaji wa ndani na kimataifa kupata thamani ya kiuchumi.

Likiwa limezinduliwa mwaka 2022, hili ni Toleo la 5 la SB ATB. Toleo la 1,2,3 na 4 yalichapishwa Juni 2022, Novemba 2022, Mei 2023 na Agosti 2024 mtawalia. SB ATB inaangalia zaidi nchi 10: Angola, Ghana, Kenya, Msumbiji, Namibia, Nigeria, Afrika Kusini, Tanzania, Uganda na Zambia.

**Madhumuni ya SB ATB ni kutoa uchambuzi madhubuti na wa kina ambao unaweza kwa kisomi kueleza na kukuza mfumo ekologia wa biashara Afrika.**

**Zikiboreshwa kila mwaka data zimewawezesha wadau kupima mapigo ya biashara ya Afrika katika muda sahihi kupima maboresho au kushuka kwa imani ya biashara, kufuatilia changamoto za kitendaji na kuanisha mabadiliko katika ufanyaji biashara kwa jumla.**

**SB ATB inatokana na vyanzo vya data ya msingi na ya pili.** Utafiti wa msingi unatokana na mapitio ya zaidi ya makampuni 2240 yanayowakilisha biashara ndogo, kubwa na makampuni kwenye hizo nchi 10. Uchunguzi umeboreshwa na mahojiano ya kina na viongozi teule katika nchi zinazohusika, na data ya pili kutoka vyanzo kama Benki ya Dunia, Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) na Benki Kuu na nchi husika.

Kuongeza taarifa za nchi zinazohusika, taarifa iliyounganishwa itachapishwa itumike kama jiwe la msingi la barometa ya biashara.

Waraka huu utachambua data kutoka mtazamo linganishi wa mambo yanayowezesha na kukuza biashara kwenye masoko ya nchi 10 za Kiafrika zilizochunguzwa.

**Hii ni Ripoti ya nchi ya Tanzania**

Inajumuisha uchambuzi wa data ya msingi na ya pili iliyokusanywa maalumu kwa Tanzania na inaonyesha mienendo na fursa katika biashara ndani ya nchi. Data ya msingi na ya pili ilikusanywa Tanzania kati ya Septemba, 2024 na Oktoba 2025 kwa ajili ya Toleo hili la tano la SB ATB.

## Jumla ya biashara 190 zilipitiwa Tanzania

Biashara zilizopitiwa Tanzania zilikuwa katika majiji au mijii: Dar es Salaam, Mwanza, Arusha, Mbeya na Moshi.Ili kupata uwakilishi, nyingi ya biashara hizi (68%) zilikuwa biashara ndogo (angalia Jedwali 1) kwa kuwa biashara nyingi ziko chini ya kundi hili. Kulikuwa na mahojiano matatu ya kina yaliyofanywa Tanzania kama sehemu ya Toleo hili. Hayo yalifanyika na wawakilishi kutoka Benki Kuu ya Tanzania, Wizara ya Fedha na Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania.

Biashara ndogo Biashara kubwa Ushirika Chanzo:

Barometa ya Biashara ya Afrika ya Benki ya Stanbic, Toleo la 5

Ukweli kwamba biashara nyingi zilizofanyiwa utafiti ni biashara ndogo ni moja ya faida kubwa ya Barometa ya Biashara ya Afrika ya Stanbic Bank (SB ATD). Kwa kawaida jumla ya data ya biashara na taarifa kuhusu Bara la Afrika zinakinzana na biashara kubwa zinazohusiana na bidhaa maalumu kwa wingi. Kwa hiyo aghalabu shughuli na tabia za utendaji biashara wa biashara ndogo haziwakilishwi vizuri.

## Ukinzani kuhusu biashara ndogo wa SB ATB.

Msisitizo na matokeo katika SB ATB yanahusu biashara ndogo, mwenendo, shughuli na mitazamo yao juu ya biashara. Aidha SB ATB inachangia katika kuelewa mitazamo ya kibiashara ya biashara ndogo Afrika ambazo sio lazima zihusiane na biashara ya mpakani. Uelewa wa mitazamo ya biashara zote ndogo ni ufunguo kwa vile unasaidia safari ya Afrika kutoka mparaganyiko wa mawanda ya biashara hadi ulioimarika ambako idadi kubwa ya washirika wa kiuchumi wameshiriki katika biashara baina yao.

**Angalizo:** Matokeo mengine ya utafiti katika ripoti hii yanaweza kutofautiana na data katika kiwango cha jumla kwa vile data katika kiwango cha jumla inapingana na biashara kubwa chache zinazoshughulikia idadi kubwa ya bidhaa. Hii inaonyeshwa kuwa ni muhimu katika ripoti hii.

**Jedwali: Mgawanyiko** wa uchunguzi wa biashara Tanzania kwa vipande






# 2 2. BENKI YA STANBIC AFRICA BAROMETA YA BIASHARA TOLEO LA 5 VIWANGO VYA NCHI

Tanzania ilibaki nafasi ya 4 katika viwango vya Barometa ya Biashara ya Afrika Benki ya Stanbic.

**Ili kutayarisha kielezo cha Viwango cha Barometa ya Biashara (SB ATB) ya Benki ya Stanbic Afrika aina za kimada kuu saba za data zinakusanya kutoka vyanzo vya data ya msingi na ya pili. Aina hizi za kimada ni mazingira ya kiuchumi mkuu, uimara wa uchumi mkuu, msaada wa Serikali, vikwazo vya miundombinu na uwezeshaji, uwazi wa biashara, tabia ya kifedha ya biashara na upatikanaji wa fedha, biashara ya nje na ufanyaji biashara Afrika. SB ATB ina viwango vya biashara viwili vifuatavyo:**

- Barometa ya Wingi wa Biashara ya miaka 3 ya Benki ya Stanbic SB QTB) inatokana na mtazamo wa utafiti wa pili. Alama na viwango vya SB QTB kwa nchi ni wastani wa viashiria vyote vilivyochaguliwa kutoka vyanzo vya data ya pili inayopatikana na taarifa mbalimbali.
- Barometa ya Biashara ya Mapitio ya Kampuni ya Benki ya Stanbic (SB STB) inatayarishwa kutokana na mtazamo wa data ya msingi. Alama na viwango vya SB STB kwa kila nchi ni wastani wa mapitio ya data yote iliyokusanywa kutoka biashara 2218.

**SB ATB ni mkusanyiko wa SB na QTB na SB STB. Mabadiliko katika viwango vya nchi kwenye vielezo vitatu (SB ATB, SB QTB na SB STB) vinasukumwa na mabadiliko kwenye wastani wa alama kwa nchi inayohusika pamoja na nafasi yao kwa jumla kulingana na nchi nyingine zote kwa Pamoja. Mabadiliko katika viwango vya SB ATB kwa mwaka uliopita vinasukumwa zaidi na mabadiliko katika alama kwenye SB STB.**

**Viwango vya nchi vya SB ATB ni linganishi kwa vile nchi zinalinganishwa dhidi ya nyingine yaani alama linganishi dhidi ya kila nchi.**

Hii inawekwa kwenye kipimo cha 0-100. Ikiwekwa kwenye kipimo hiki Msumbiji ina Kielezo cha Biashara cha juu zaidi wakati Zambia ikiwa ya chini kabisa. Hii haina maana kuwa mtu hawezi kufanya biashara Zambia au Msumbiji imekamilikwa. Ina maana tu kwamba kwa nafasi

kuanzia ya 0 na alama ya juu ya 100, hivi ndio ambavyo masoko hayo mawili yalivyoonekana.

**Tanzania kushikilia nafasi ndani ya 50% za juu za viwango vya ATB inaakisi mitazamo chanya ya biashara kuhusu ubora wa miundombinu, uthabiti wa biashara mintarafu uchumi na msaada wa serikali kwa biashara. Hata hivyo changamoto zinabaki hususan katika mitazamo ya masharti ya mikopo yanayotolewa kwa wateja.**

**Jedwali Z:** Viwango vya ATB, QTB na STB kwa nchi.

1=Alama ya juu ya ufanyaji biashara — 10=Alama ya chini ya ufanyaji biashara

| ATB | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Okt '25 | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | 9 | 10 |
| Agos '24 | 3 | 1 | 2 | 4 | 5 | 7 | 6 | 10 | 9 | 8 |
| Mei '23 | 3 | 1 | 2 | 7 | 4 | 5 | 6 | 10 | 8 | 9 |

| QTB | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Okt '25 | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | 9 | 10 |
| Agos '24 | 3 | 1 | 2 | 4 | 8 | 5 | 7 | 6 | 9 | 10 |
| Mei '23 | 3 | 1 | 2 | 4 | 5 | 6 | 8 | 7 | 9 | 10 |

| QTB | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Okt '25 | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | 9 | 10 |
| Agos '24 | 1 | 3 | 2 | 4 | 7 | 5 | 8 | 6 | 9 | 10 |
| Mei '23 | 2 | 1 | 4 | 3 | 8 | 7 | 5 | 9 | 6 | 10 |

Kiwango kilichoboreka — Kimebaki katika kiwango kilekile — Imeshuka katika kiwango

**Ufunguo:** Angola Ghana Kenya Msumbiji Namibia Nigeria Afrika Tanzania Uganda Zambia Kusini

**Chanzo:** Barometa ya Biashara ya Afrika ya Benki ya Stanbic, Toleo, 5

**Maelezo:** Viwango vyote vimeonyeshwa ili kiwango cha juu ni kizuri kwa biashara, wakati kiwango cha uchumi cha juu kabisa na cha chini vikipangwa kama 1,2,3 n.k, na namna hali hii ilivyobadilika nyakati tofauti. Alama nyekundu inaonyesha nchi imeshuka katika kiwango kinachohusika kutoka Agosti, 2024.

**Jedwali 3:** Washirika wakubwa katika mawanda yote matano ya SB ATB (Juni 2022-Octoba 2025)




**Jedwali 4:** Alama na nafasi za ATB ya Tanzania (Juni 2022 - Oktoba 2025)




Tanzania imefungana na Msumbiji na Angola kwa wimbi kubwa zaidi la mafanikio makubwa ya SB ATB, Tangu Juni 2022 wakati Tanzania ikishika nafasi ya 6 katika SB ATB imeimarika kwa kupanda hadi nafasi ya 4 katika msimamo wa uchunguzi wa hivi karibuni (angalia Jedwali 3). Namibia na Nigeria pekee ndiyo zimepata mafanikio makubwa zaidi katika uchunguzi.

Pamoja na kubaki na nafasi yake ya SB ATB katika msimamo huu wa uchunguzi alama ya mfanyabiashara wa Tanzania imeendelea kukua tangu Septemba, 2023.

Katika kipindi cha miaka mitatu ya uchunguzi kilichopita alama ya kibiashara ya Tanzania imekuwa zaidi ya mara mbili, kutoka 15 Mei 2023 hadi 31 Octoba 2025. Matokeo yake Tanzania imeimarika kwa nafasi tatu katika viwango vya SB ATB- kutoka nafasi yake ya chini kabisa (7) Mei 2023 hadi nafasi ya 4 Agosti. 2024 na Octoba 2025 (Angalia Jedwali 4).

Mafanikio ya Tanzania kwa kiasi kikubwa yamesukumwa na utendaji wake katika SB STB.

Kihistoria,Tanzania imekuwa ndiyo mtekelezaji madhubuti zaidi katika viwango vya SB STB ikiwa imepata nafasi ya 1 katika misimamo mitano ya utafiti Tanzania ilishika nafasi ya 1 katika viwango vya SB STB Septemba 2022, Agosti 2024 na Octoba 2025. Katika misimamo mingine yote ya utafiti, Tanzania bado ilibaki katika 50% ya nafasi za SB STB. Utendaji huu unaakisi mitazamo chanya endelevu katika biashara za Tanzania zilizochunguzwa hasa biashara ndogo'biashara zilizochunguzwa kuhusu mawanda ya biashara za Tanzania. Biashara zilizochunguzwa zinaona uwezekano wa ukuaji wa uagizaji, kujiamini kama shughuli ya utendaji wa kiuchumi, ubora wa biashara na miundombinu inayohusiana na usafiri, vikwazo vya miundombinu inayohusiana na usafiri, vikwazo vya miundombinu vinavyoathiri biashara, kanuni za ushuru za nchi kwa waingizaji na waagizaji, kushika nafasi ya 1 katika vipimo hivi katika misimamo mitatu ya SB STB.

Licha ya utendaji mzuri katika SB STB, Tanzania imeendelea kushika nafasi ya Chini 50% ya SB QTB.

Tangu iliposhika nafasi yake ya juu kabisa (5) Juni 2022, nafasi ya Tanzania imeshuka nafasi mbili hadi 7 Agosti 2024 na Octoba 2025. Kushuka kwa Tanzania katika kiwango cha SB QTB inaakisi kushuka kwake kwenye alama SB QTB kutoka 57 Juni 2022 hadi 16 Octoba 2025 (Angalia Jedwali 5). Tanzania ilikuwa ya mwisho katika mfumuko wa bei na biashara za masharti ya mikopo zimefika kwa wateja katika misimamo mitatu ya SB QTB. Viashiria vingine muhimu vinavyoathiri vibaya alama za SB QTB za Tanzania inajumuisha biashara ya bidhaa kama asilimia ya GDP, ambapo ilishika nafasi ya 9, halafu ilishika nafasi ya 8 katika uagizaji wa bidhaa na huduma kama asilimia ya GDP, kiwango cha ubadilishaji rasmi cha nchi na viwango vya ushuru. Hata hivyo Tanzania imeonyesha maboresho ya wastani kuanzia Mei, 2023 wakati iliposhika nafasi yake ya SB QTB ya chini kabisa ya 8. Maboresho ya Tanzania hadi nafasi ya 7 Agosti 2024 na Octoba 2025 inaakisi utendaji madhubuti katika wastani wa miaka 3 wa usajili wa simu za mkononi kwa watu 100 na ya 1 na 2 mtawalia katika vipimo hivi. Sehemu iliyobaki ya ripoti hii inaonyesha utendaji wa Tanzania katika Barometa ya Biashara Afrika ya Benki ya Stanbic Toleo la 5 kwa mtazamo wa msingi na wa pili, kulingana na maeneo makubwa ya kimada yaliyorejewa awali.

Jedwali 5: Alama za Tanzania SB na SB STB (Juni 2022-Oktoba 2025)




Chanzo: Barometa ya Biashara Afrika ya Benkiy a Stanbic Toleo 5



# 3 MAZINGIRA YA UCHUMI MKUBWA

Mazingira ya uchumi mkuu wa nchi yana nafasi kubwa katika kutengeneza mvuto wa biashara wa jumla, uwekezaji na shughuli za biashara.

Sababu ambazo kwa kawaida zinakuza mvuto wa taifa kwa wawekezaji ni pamoja na Pato la Taifa (GDP), linaloonyesha uzalishaji wa kiuchumi mkubwa, ukuaji wa Pato la Taifa kwa mtu unaoakisi uwezo madhubuti wa mtumiaji, mfumuko wa bei mdogo, na sarafu imara ambayo inatoa athari chanya kwa mvuto wa biashara wa nchi. Na zaidi viwango vya juu vya uwekezaji wa kigeni wa moja kwa moja (FDI) unaonyesha msaada kwa mazingira ya biashara, ambapo kiasi cha kutosha cha biashara ya bidhaa kuhusiana na GDP kinaonyesha biashara imara ya mipakani na muungano wa masoko ya dunia.

Muonekano wa kiuchumi wa Tanzania unabaki kuwa imara ukisaidiwa na juhudi za kukuza uimara wa uchumi mkuu

Uboreshaji katika uthabiti wa nje na kuimarika taratibu kwa sekta muhimu kunaongoza ukuaji wa kiuchumi ndani ya nchi. Ukuaji halisi wa GDP ulikadiriwa kuwa 5.9% mwaka 2025 hadi 5.6% mwaka 2024 na inakadiriwa kuongezeka zaidi hadi 6.4% mwaka 2026 ikionyesha uchumi imara na unaokua (angalia Jedwali 1). Mtazamo huu unaonyesha ongezeko kutoka miaka ya karibu iliyokuwa na ongezeko la wastani na changamoto.

Uchaguzi mkuu wa Octoba 2025 ulitokea kwa kuchaguliwa tena Rais Samia Suluhu Hassan aliyeshinda muda wake wa kwanza wa miaka mitano kwa ushindi mkubwa wa 97.65% ya kura. Ushindi huu mkubwa wa sera zake za utawala, kuendeleza miradi ya miundombinu mikubwa na kuangalia ukuaji wa viwanda. Kwa jumuia ya biashara ridhaa hii ya uchaguzi inaonyesha sera za muda mrefu na kuimarisha mwelekeo kwenye ushirikiano wa kikanda na mageuzi ya kimuundo yanayolenga kuimarisha mazingira ya biashara ya taifa.

Ukuaji wa kiuchumi mwaka 2025 ulisaidiwa na kilimo, huduma na sekta za viwanda

Serikali inaendelea kuimarisha maeneo haya kupitia uwekezaji wa miundombinu uliolengwa na mageuzi ya sera yaliyolenga kuimarisha upatikanaji wa nishati na usafiri. Hii inathibitishwa na utendaji wa uchumi katika robo ya tatu ya waka 2025 ambapo Kielezo cha Uzalishaji Viwandani (11P) kilipanda hadi 113.9 ongezeko la 7% kutoka robo iliyopita kwenye uzalishaji wa tumbatu na ongezeko la 16% katika metali za msingi. ,

Sekta ya huduma ilibaki kuwa muhimu kwa jumla ya mapato ya uuzaji nje kufika Dola za Kimarekani bilioni 17 kwa mwaka ulioishia Septemba, 2025 ukiimarishwa na ongezeko la 12% ya watalii na usafirishaji, hususan mizigo uliofikia Dola za Kimarekani bilioni 2.5.

Ukuaji mzuri uliimarishwa zaidi na sekta za madini na utalii ambazo kwa kiwango kikubwa zimekuza akiba ya fedha za kigeni na GPD kwa jumla. Sekta ya madini ilipata mafanikio ya kihistoria kwa kuchangia 10% kwenye GDP mwaka 2024 na kufikia lengo lake kitaifa miaka miwili kabla ya ratiba na hisa zake ziliimarika kati ya 9.5% na 10% mwaka wote wa 2025.

Usafirishaji madini, ukitawaliwa na dhahabu ulichangia takriban 50% hadi 55% ya jumla ya uuzaji nje wa taifa 2025 kwa mapato yaliyovunja rekodi ya bilioni 4.43 ya Dola za Kimarekani kwa mwaka unaoishia Septemba, 2025.

Mapato haya yalisaidia kukuza akiba ya fedha za kigeni hadi Dola za Kimarekani bilioni 6.66 hadi mwisho wa Septemba 2025-yatosha kulipia zaidi ya miezi mitatu ya uagizaji uliokadiriwa. Kwa pamoja tasnia ya utalii ilipata kipato chake cha juu kabisa cha Dola za Kimarekani bilioni 4.2 hadi Oktoba 2025 zikisukumwa na wageni wa kimataifa milioni 2.09, ongezeko la 9% kwa mwaka. Utendaji huu wa kipekee katika madini na utalii ulisaidia kupunguza nakisi ya fedha ya sasa hadi kufikia takriban 2.2% hadi 2.3% ya GDP. Wakati huo huo kilimo kiliendelea kuimarika, ikiweka kiwango cha ukuaji 4% na kuhakikisha usalama wa chakula ambao uliweka mfumuko wa bei katika wastani wa 3.4% hadi Septemba, 2025.

Mapato haya yalisaidia kukuza akiba ya fedha za kigeni hadi Dola za Kimarekani bilioni 6.66 hadi mwisho wa Septemba 2025-yatosha kulipia zaidi ya miezi mitatu ya uagizaji uliokadiriwa. Kwa pamoja tasnia ya utalii ilipata kipato chake cha juu kabisa cha Dola za Kimarekani bilioni 4.2 hadi Oktoba 2025 zikisukumwa na wageni wa kimataifa milioni 2.09, ongezeko la 9% kwa mwaka. Utendaji huu wa kipekee katika madini na utalii ulisaidia kupunguza nakisi ya fedha ya sasa hadi kufikia takriban 2.2% hadi 2.3% ya GDP. Wakati huo huo kilimo kiliendelea kuimarika, ikiweka kiwango cha ukuaji 4% na kuhakikisha usalama wa chakula ambao uliweka mfumuko wa bei katika wastani wa 3.4% hadi Septemba, 2025.

Shinikizo la mfumuko wa bei nchini Tanzania kwa wastani linabaki chini lakini inategemea kupata upandaji mdogo katika kipindi cha hivi karibuni ikichochewa na mishtuko ya nje na mienendo ya kifedha ya nyumbani Kiwango cha mfumuko wa bei kilikadiriwa kuwa wastani wa 3.1% mwaka 2024 na ilikadiriwa kuweza kuongezeka kwa wastani hadi 3.4% mwaka 2025 na kukadiriwa kuendelea kuongezeka hadi 3.6 (angalia Jedwali 1).

**Jedwali 1:** Viashiria vya Uchumi Mkuu Vilivyoanishwa kwa Tanzania vyenye athari kwenye mvuto wake wa kibiashara.

| Kiashiria | Kiasi | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025e | 2026f |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Pato la taifa kwa majina | USD, Mabilioni | 62.8 | 67.8 | 73.4 | 77.5 | 80.6 | 89.4 | 98.9 |
| Pato la taifa kwa kila mtu | USD | 1 157 | 1 213 | 1 272 | 1 256 | 1 215 | 1 312 | 1 451 |
| Kiwango cha ukuaji halisi wa Pato la Taifa | % | 4.8 | 4.8 | 4.7 | 5.1 | 5.5 | 5.8 | 6.1 |
| Kiwango cha mfumuko wa bei | % | 3.3 | 3.7 | 4.4 | 3.7 | 3.1 | 3.4 | 3.6 |
| Kiwango cha riba ya ukopeshaji | % | 15.7 | 16.8 | 16.8 | 16.5 | N/A | N/A | N/A |
| Mizania ya Biashara | USD bilioni | 21.9 | -1.8 | -5.1 | -6.0 | -5.2 | -4.6 | -5.1 |
| Kiwango cha ubadilishaji | TZS kwa USD | 2 313.6 | 2 303.8. | 2 327.1 | 2435.5 | 2582.5 | 2544.6 | 2529.7 |
| FDI | USD, Mabilioni | 0.9 | 1.2 | 1.4 | 1.6 | 1.7 | 1.8 | 2.2 |
| Biashara ya usafirishaji nje na uagizaji kama % ya GDP | % | 28 | 30 | 35 | 38 | 42 | N/A | N/A |

**Ripoti Iliyofichuliwa ya Masoko ya Afrika ya Standard Bank (Juni 2025), Benki ya Dunia, Benki ya Tanzania, Wizara ya Fedha, Ofisi ya Kitaifa ya Takwimu**

**Maelezo:** f ina maana ya alama ya makadirio ya data: Taarifa iliyokusanywa ni mpaka Juni 2025 na utabiri ungeweza kurekebishwa wakati wa uchapishaji.

Benki Kuu ya Tanzania iliendelea na sera ya kiwango takriban 5.9% mwaka 2024 na kubaki nacho hadi 5.75% hadi Desemba 2025 kuzuia mategemeo ya mfumuko wa bei na kubaki na uthabiti wa kiwango cha ubadilishaji. ,

Njia ya mfumuko wa bei ya Tanzania inaonekana kudhibitika kama masoko mengine yanayochipuka yakitekeleza sera za fedha kwa tahadhari katika hofu ya kidunia.

Kuangalia msukumo uliovunja rekodi wa Uwekezaji wa Moja kwa Moja wa Kigeni (FDI) Afrika nzima ambao ulifikia kiwango cha juu cha muda wote cha Dola za Kimarekani Bilionii 97 mwaka 2024. Tanzania inajivunia kasi hii. Ikisukumwa na mfumo huria na juhudi za uwekezaji ambazo zilikuza mapato ya Afrika kwa 75%, FDI ya Tanzania inalengwa kufikia USD bilioni 1.8 mwaka 2025 na mwaka 2026.

Ukuaji huu wa uhakika unaakisi kuboresha mazingira ya uwekezaji nchini. Kufurahia mafanikio haya malipo binafsi ambayo yalifikia 1.0% ya GDP mwaka 2024 yanaendelea kutoa safu imara kwa akaunti za kigeni za Tanzania na kuimarisha uthabiti wa kifedha wa taifa katika uchumi wa kikanda unaokua.

Sekta ya kigeni pia inategemea kuonyesha uthabiti na uboreshaji wa taratibu mwaka 2024. Akiba ya biashara ya nchi imeonyesha ukuaji ikisukumwa na mauzo ya nje kama madini, bidhaa za kilimo, na utengenezaji wa bidhaa. Dhahabu inabaki kuwa madini makubwa ya kuuza nje, wakati mauzo ya nje ya asili kama tumbaku na korosho yaliongezeka kwa 25% kutokana na ongezeko la bei na ukubwa wake mwaka 2025.

Uuzaji wa nje wa bidhaa na huduma wa Tanzania ulitegemea kufikia USD bilioni 17 mwaka 2025 na USD bilioni 18 mwaka 2026. Hata hivyo uingizaji wa nchi umeongezeka kwa kiasi kikubwa na nakisi ya biashara ikitarajiwa kuongezeka kimsingi ikisukumwa na miradi ya miundombinu yenye kuhitaji mitaji mikubwa kama vile reli ya kisasa (SGR) na Kituo cha Kufua Umeme kwa Maji cha Julius Nyerere pamoja na ukuaji wa mahitaji ya vifaa vya viwandani. ,

Nchi, kwa kiasi ina sera ya biashara huria, wakati biashara kama 42% ya makadirio ya GDP ikitegemewa kuongezeka pamoja na ukuaji wa kiuchumi.

Muonekano wa kifedha wa Tanzania una sifa ya wasifu thabiti wa deni. Kuanzia mwaka 2024, deni la nje lilikua takriban 32% ya GDP ambalo wakati huo lilitegemewa kushuka hadi 30% mwaka 2025. (Angalia Jedwali 6). Makadirio kwa mwaka 2026 ni kwamba deni la nje linaweza kuwa takriban 31% ya GDP kusaidia lengo la Tanzania kuwa na udhibiti wa deni katika ukuaji wa uchumi unaoendelea. Serikali inaendelea kulenga kwenye uimara wa uchumi mkuu na usimamizi wa madeni, unaolenga uwiano wa ukopaji wa nje na jitihada za mapato ya ndani, na kutoa athari chanya kwa mvuto wa biashara ya Tanzania kwa kuimarisha Imani ya uwekezaji na kuhakikisha uimara wa kifedha.

**Jedwali 6:** Deni la Tanzania (la ndani na nje) kama% ya GDP




**Chanzo:** Ripoti iliyoachiliwa ya Standard Bank ya Masoko ya Afrika Juni 2025

**Maelezo:** 'f' inawakilisha alama za data zinazotabiriwa; 'e' inawakilisha alama ya data zinazokadiriwa.

Soko la fedha za kigeni la Tanzania linategemewa kupata mshuko wa thamani wa taratibu wa Shillingi ya Kitanzania (TZS), kuonyesha marekebisho ya soko katikati ya mazingira ya dunia na ya ndani. Shillingi ya Tanzania ilitegemewa kufanya biashara katika wastani wa TZS 2,655.9 kwa Dola ya Kimarekani mwaka 2025 na kukadiriwa kwa wastani wa TZS 2,718.9 kwa Dola ya Kimarekani mwaka 2026 na kufanya mshuko wa taratibu kutoka TZS 2,435.5 mwaka 2024. Licha ya shinikizo hilo la chini kwenye thamani ya sarafu, nafasi ya uwezo wa kifedha wa Tanzania inabaki imara wakati akiba ya fedha za kigeni ikitegemea kukua kwa kiasi kikubwa, kutoka bilioni 5.7 za Dola za Kimarekani mwaka 2024 hadi makadirio ya Bilionii 6.4 za Dola za Kimarekani mwaka 2025 na kufikia makadirio ya Bilionii 7.0 ya Dolla za Kimarekani hadi mwisho wa 2026. Ukuaji huu katika akiba unaonyesha kwamba wakati kiwango cha ubadilishaji kinajirekebisha na nguvu ya soko Benki ya Tanzania (BOT) kwa mafanikio inaimarisha bafa yake kudumisha uimara wa uchumi mkubwa kwa jumla na kusaidia sera ya fedha ya tahadhari. Ili kuhakikisha kwamba sekta binafsi inayokua, ambayo ukuaji wa mtaji wake ulifika 20.3 mwaka 2025, ina uwekezaji wa fedha wa kutosha BOT imesimamia vizuri ukwasi wa soko kupitia mfumo wake wa viwango vya riba. Kwa kushusha kiwango cha Benki Kuu (CBR) hadi 5.75% Oktoba 2025 na kutumia nyaraka kama vile mikataba ya dhamana ya kurudisha, BOT imefanikiwa kutekeleza mahitaji makubwa ya fedha kutoka benki za biashara wakati ikisimamia riba kati ya benki katika ukanda imara. Uingiliaji huu umesaidiwa na mageuzi ya kimuundo pamoja na marekebisho ya mfumo wa usimamizi wa Msaada wa Dharura wa Ukwasi (ELA) ulioandaliwa kuhakikisha mfumo wa upatanishi wa kifedha mzuri unaoweza kusaidia nia ya ukuaji ya Tanzania kwa 6%.

Kwa jumla Tanzania inanufaika na misingi yake ya uchumi mkubwa pamoja na ukuaji mzuri wa uuzaji nje hasa kwenye madini na bidhaa za kilimo, na ongezeko la uwekezaji wa moja kwa moja wa kigeni ambavyo kwa pamoja vinakuza mvuto wa biashara wa nchi.



# 4 UIMARA WA UCHUMI MKUU

Mfumo wa sera za kimkakati huongeza matarajio ya mazingira ya biashara ya muda mrefu Tanzania.

## KIWANGO CHA KIELEZO CHA KUJIAMINI KWA BIASHARA CHA TANZANIA




**Chanzo:** Barometa ya Biashara ya Afrika ya Benkiy a Stanbic Toleo 5

Kujiamini kwa biashara kunaweza kubadilika kati ya 0 na 100 ambapo 0 inaonyesha kutojiamini kabisa, 50 katikati vna 100 kujiamini kabisa.Katika matokeo ya utafiti wa Oktoba 2025 SB ATB kiwango cha kielezo cha kujiamini kwa biashara cha Tanzania kiliongezeka kidogo hadi 73 kutoka 72 katika utafiti wa ATB wa mwezi Agosti 2024.

Kiasi cha biashara zilizofanyiwa utafiti ambazo zilikuwa na matumaini makubwa au matumaini makubwa mno kuhusu utendaji wa uchumi mintarafu biashara zao katika miaka 3 ijayo kiliongezeka kwa pointi ya asilimia 8 hadi 74% kutoka 66% mwezi Agosti 2024 (Angalia Mchoro 7). Biashara ndogo zilizofanyiwa utafiti zilifuata mtindo huu- ikiongezeka kwa asilimia ya point 17 katika kipindi hicho hicho. Kwa hiyo basi kiasi cha biashara zilizofanyiwa utafiti ambacho hawakuwa na mategemeo makubwa au kutokuwa na matumaini kabisa kilipungua kutoka 2% kutoka 10% katika kipindi hicho hicho. Hii inaashiria kwamba sehemu kubwa ya biashara zilizochunguzwa ambazo awali ziliionyesha hofu zilihamia katika matumaini katika msisitizo huu wa utafiti (Angalia Mchoro 7).

**Mchoro 7:** Mtazamo wa biashara za Tanzania zilizofanyiwa utafiti kuhusu utendaji wa uchumi mintarafu biashara.




**Chanzo: Barometa ya Biashara ya Afrika ya Benki ya Stanbic, Toleo la 5**

**Angalizo:** 'Iliyokataliwa' haijaonyeshwa kwenye slaidi. Ukomo unaweza usifike 100% kamili.

Imani ya biashara zilizochunguzwa kuhusu uchumi imeongezeka katika mawimbi manne ya SB ATB yaliyopita (Angalia Mchoro 8). 74% ya biashara zilizochunguzwa zilionyesha matumaini makubwa (ama matumaini makubwa au matumaini mno) katika msisitizo huu wa utafiti kulingana na 66% mwezi Septemba 2022. Hii imesukumwa kwa kiasi kikubwa na mwenendo kama huo miongoni mwa biashara ndogo ambazo zilichunguzwa ambazo ziliarifu ongezeko la asilimia pointi 11 kwa kipindi hicho hicho..

**Mchoro 8:** Sehemu ya biashara za Tanzania zilizochunguzwa ambazo zinaonyesha matumaini katika utendaji wa uchumi katika mapitio 4 yaliyopita ya SB ATB.




**Chanzo:** Barometa ya Biashara ya Afrika ya Benki ya Stanbic

Biashara zilizochunguzwa pia zina matumaini kuhusu ukuaji wa biashara zao, kwa sababu mbalimbali. 71% ya biashara zilizochunguzwa zilionyesha ukuaji wa biashara kama kichocheo cha mtazamo wao chanya katika msisitizo wa utafiti, ongezeko la asilimia kumi (10) za pointi kutoka Agosti 2024. Maelezo kuhusu masharti makubwa kutoka kwa wateja wa biashara ambazo

> Kuna mwelekeo wa ukuaji unaoonekana katika biashara ya kimataifa kama matokeo ya sera za biashara zinazounga mkono na mifumo wezeshi. Mifumo yetu sasa ni rahisi kufikia na kutumia kwa sababu imeunganishwa.
>
> Mwakilishi kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania

zimechunguzwa pia waliona ongezeko kubwa la asilimia 24 za pointi; na kupanda hadi 61% katika kipindi hicho hicho. Pamoja na hayo biashara zilizochunguzwa zimeeleza ushukaji katika mambo mengine. Matumaini yaliyotokana na ongezeko la ukuaji wa kiuchumi yalipungua hadi 28% kutoka 30% Agosti, 2024 wakati uimara wa kiuchumi na sera nzuri ulishuka hadi 14% kutoka 26% na 31% mwezi Agosti, 2024 mtawalia. Kwa hiyo mategemeo ya mabadiliko ya Serikali kuchochea uchumi yalionyesha punguzo dogo kutoka 24% hadi 21% katika kipindi hicho hicho.

"Kuna mwenendo wa ukuaji wa wazi wa biashara ya kimataifa kutokana na msaada wa sera za biashara na mafunzo wezeshi. Sasa mifumo yetu ni rahisi kuipata na kutumia kwa vile imeunganishwa."

Miwakilishi kutoka Mamlaka ya Kodi Tanzania.

Sanjari na matumaini makubwa yaliyoonyeshwa na biashara zilizochunguzwa, ukuaji wa GDP halisi unategemea kuendelea kuongezeka ukionyesha mwenendo wa kiuchumi mpana ambao utanufaisha biashara. (Angalia Mchoro 9). Ukuaji huu unategemea kufikia 5.8% mwaka 2025 ongezeko kutoka 5.5% mwaka 2024, na inategemewa kuongezeka zaidi hadi 6.1% mwaka 2026. Ukuaji wa kiuchumi unaendelea sambamba na mazingira ya mfumuko wa bei ambao umezuiwa kwa wastani licha ya kuongezeka taratibu kwa kiwango cha mfumuko wa bei kukadiriwa kwa wastani wa 3.4% mwaka 2025, ongezeko kutoka 3.1% mwaka 2024 na inategemewa kuongezeka kidogo hadi 3.6% mwaka 2026. Licha ya ukuaji huu mdogo viwango hivi vya bei vya wastani vinaendelea kusaidia uwezo halisi wa ununuaji wa watumiaji, ikitoa njia nyeupe kwa biashara kufikia viwango vyao vya ukuaji kupitia kiasi cha mauzo endelevu. Msingi wa uvumilivu wa uchumi unaonekana zaidi kwa uimarishaji wa sekta ya nje na uthabiti wa kifedha. BOT ilieleza kwamba akiba ya fedha za kigeni ilibaki madhubuti kiasi cha Bilionii 6 za USD mwisho wa Octoba 2025 inayotosha kwa miezi 4.7 ya uagizaji wa bidhaa na huduma unaotarajiwa, ikipita vigezo vyote vya kitaifa na Jumuia ya Afrika Mashariki.

Uimara katika akiba kwa kiasi unakuwa bafa kwa biashara zinazohusika na biashara ya kimataifa, ikipunguza hatari ya kuyumba kwa sarafu ambako aghalabu huharibu hisia za muda mrefu za "sera nzuri". Zaidi ya hapo sekta ya benki imeonyesha hali nzuri sana inayoakisiwa katika muendelezo wa ukuaji wa mwaka wa mikopo ya sekta binafsi ambapo ilikua kwa 16% mwezi Oktoba 2025, kimsingi ikisukumwa na shughuli nyingi katika uchimbaji madini na kokoto, kilimo, hoteli na migahawa. Aidha ukwasi kutoka mfumo wa benki ulibaki toshelevu, ambapo kiwango cha riba katika soko la fedha baina ya benki kikipungua hadi 6.38% mwezi Oktoba 2025. Uboreshaji katika ubora wa mikopo unaonyesha kwamba asasi za kifedha ziko katika nafasi imara zaidi kukopesha biashara zinazotaka kukua.

**Mchoro 9**: Ukuaji sahihi wa GDP ya Tanzania(%)




**Chanzo:** Standard Bank, 2026, Ripoti iliyoachiwa ya Masoko ya Afrika, Januari, 2026

**Maelezo:** 'f' inawakilisha alama ya data iliyotabiriwa, na 'e' inawakilisha alama ya data inayokadiriwa.

Maendeleo haya katika malipo ya kidigitali yamekutana na upungufu katika matumizi ya fedha. Matumizi ya fedha katika ununuaji katika biashara ya mpakani yalipungua yakifanya kama 18% tu ya mauzo ya biashara ya mpakani katika utafiti huu kulinganisha na 23% mwezi Agosti, 2024.

Biashara ya mpakani katika utafiti huu kulinagnisha na 23% mwezi Agosti, 2024

**Mchoro 20:** Njia ya malipo inayopendelewa kwa unuwaji wa mpakani




**Chanzo:** Barometa ya Biashara ya Afrika ya Benki ya Stanbic, Toleo la 5

**Maelezo:** Nyingine ni pamoja na hati za mkopo na njia nyingine za malipo.

40% ya ununuaji wa biashara ya mipakani katika biashara zilizofanyiwa utafiti ulifanyika kwa kadi kulinganisha na 30% mwezi Agosti,2024

Agizo la Benki Kuu ya Tanzania kupitisha uhamishaji wa fedha wa kimataifa kupitia tu mfumo wa Ulipaji wa Haraka (TIDS) kuanzia Agosti,2025 ilirasimisha maingizo ya mpakani kwa utumiaji wa ndani wa kidigitali.

Kwa kuunganisha mikondo hii, wa kawaida ulibadilisha taratibu zilizoparaganyika na muundombinu uliounganika ambao unahakikisha ukamilikaji wa haraka na ukaguzi madhubuti kwa kila miamala .

Benki Kuu pia iliongeza ujumuishi wa kifedha wa kidigitali kwa kuweka ada za miamala baina ya akaunti za benki na "e-wallets" kuboresha ushirikiano kuanzia 1 Julai, 2025. Benki Kuu ilianzisha mfumo wa ngazi kwa uhawilishaji baina ya benki na watoaji fedha za kielektroni kufanyika upatikanaji wa huduma za kidigitali kwa kuweka ada za miamala baina ya akaunti za benki na "e-wallets" kuboresha ushirikiano. Kuanzia 1 Julai, 2025 Benki Kuu ilianzisha mfumo wa ngazi kwa uhawilishaji baina ya benki na watoaji wa fedha za kielektroni kufanikisha upatikanaji wa huduma za kidigitali za kifedha. Aidha benki na watoaji wa fedha za kielektroni walitiwa moyo kuzidi kupunguza tozo zao chini ya viwango vilivyowekwa.

Kuhusiana na miamala ya ndani, kwa upande mwingine, biashara zilizofanyiwa utafiti Tanzania zilipenda utumiaji mkubwa wa fedha wakati huo huo ikiongeza matumizi ya njia za malipo ya kidigitali. 88 na 85% za biashara ambazo zimefanyiwa utafiti Tanzania zilitumia fedha kwa uuzaji na ununuaji wa ndani katika utafiti huu mtawalia. Fedha pia zilitumika kwa 47% na 45% ya malipo ya uuzaji na ununuaji wa ndani mtawalia. Kiwango hiki kikubwa cha matumizi kinaonyesha kwamba fedha inabaki kuwa njia kuu ya malipo yanayohusiana na biashara. Hata hivyo matumizi ya malipo kwa simu kwa mauzo ya ndani yaliongezeka hadi 73 kutoka 68% mwezi Agosti, 2024. Isitoshe uwiano wa malipo ya mauzo ya ndani yaliyofanywa kupitia malipo ya simu uliongezeka vya kutosha hadi 18% kutoka 14% mwezi Agosti, 2024. Mwenendo huu ulisukumwa zaidi na ongezeko kubwa miongoni mwa biashara ndogo zilizochunguzwa. (Angalia Mchoro 21). Mwenendo huu unaonyesha kuwa wakati fedha inabaki kuwa njia ya malipo inayotumika kwa miamala ya ndani katika biashara zilizochunguzwa, uchukuaji na utumiaji wa malipo ya kidigitali, pamoja na malipo kwa simu, unakua. Matokeo ya baadaye ya utafiti huu yatatoa mwanga iwapo ukuaji wa miundombinu ya malipo ya kidigitali ungebadilisha biashara zilizochunguzwa kutoka fedha hadi njia za kidigitali:

**Mchoro 21:** Uwiano wa malipo ya mauzo ya ndani yaliyofanywa kwa simu.




**Chanzo: Barometa ya Biashara ya Afrika ya Benkiy a Stanbic, Toleo la 5**

**Sehemu kubwa ya biashara zilizofanyika utafiti ziliona upatikanaji wa mkopo ni rahisi zaidi kulingana na Agosti,2024**

Hisia za biashara zilizochunguzwa ambazo hupata mkopo zilikuwa ama rahizi kwa kiasi fulani au rahisi kabisa ziliongezeka hadi 51% kulingana na 44% mwezi Agosti, 2024 (angalia Mchoro 22). Wakati ambapo sehemu zote za biashara zilizochunguzwa ziliona upatikanaji mkopo kama rahisi zaidi katika utafit huu, kimsingi biashara kubwa na makampuni ziliongoza mwenendo huu. Biashara kubwa na makampuni ambayo yameona upatikanaji wa mkopo kama rahisi au rahisi sana iliongezeka hadi 67% na 43% mwezi Agosti, 2024 mtawalia.

**Mchoro 22:** Wepesi wa kupata mikopo




**Chanzo: Barometa ya Biashara ya Afrika ya Benki ya Stanbic**

Mitazamo hii chanya inaongezwa nguvu na mazingira ya kifedha ambayo mazuri zaidi na kufanya utaratibu wa kupata jitihada za msaada wa fedha mwaka 2025

Benki Kuu ilipunguza Kiwango cha Benki Kuu ( CBR) kwa alama za msingi 25 hadi 5.75% katika robo ya tatu ya 2025 kusaidia mahitaji ya ukwasi yanayoongezeka katikati ya mfumuko wa bei imara.

Mabadiliko haya ya sera yalitiwa mkazo na upunguaji wa taratibu wa gharama za ukopaji za kibiashara na viwango vya jumla vya ukopeshaji vikiwa takriban 15, 16% ifikapo katikati ya mwaka.

Zaidi ya hayo uzinduzi wa mwaka 2025 wa "Tanzania Youth Investment Iniatiatives" na uanzishaji rasmi wa "credit Guarantee Company" zimetoa nyenzo muhimu za kupunguza hatari kwa wakopeshaji. Hatua hizi hususan zinawanufaisha biashara ndogondogo na za kati (MSMEs) kwa kupunguza masharti ya dhamana na kukuza utoaji mtaji kwenye sekta za athari kubwa kama kilimo na biashara. Jitihada hii inaendelea na upungufu mkubwa katika biashara ndogo zilizochunguzwa ambazo zimeelezea ukosefu wa dhamana kama sababu za ugumu wao wa kupata mkopo kutoka 65% mwezi Agosti 2024 hadi 48 katika utafiti huu.

85% ya biashara ambazo zimechunguzwa zimeona kuwa kuelewa vizuri biashara zao kama sehemu ambazo asasi za kifedha zingeweza kusaidia biashara zao.

Maeneo mengine muhimu ya msaada yalijumuisha utoaji wa aina nyingi za bidhaa zinazofaa kwa mahitaji maalumu ya biashara, wepesi wa kupata fedha na utambulishwaji kwa wanunuzi wa kimataifa, kila moja ikirejewa na 85% ya wahojiwa. Aidha kutoa huduma za kihasibu na bima kukuza uimara wao wa kifedha pia ulielezwa na 85% ya biashara zilizochunguzwa.

**51%** ya biashara zilizochunguzwa ziliona upataji mkopo kuwa rahisi kulinganisha na 44% mwezi Agosti, 2024

Kwa kushughulikia mahitaji haya yaliyoonekana asasi za kifedha zinaweza kusaidia vizuri ukuaji wa urasimishaji wa biashara zote ndogo na makampuni katika Uchumi wa kidigitali unaobadilika.

# 9 BIASHARA YA NJE NA UFANISI WA BIASHARA AFRIKA

Urahisi wa biashara ya Tanzania uliongezeka ukisukumwa na upatikanaji rahisi wa masoko ya dunia licha ya ukuaji wa changamoto ndani ya Afrika..

## ALAMA ZA KIELEZO CHA URAHISI WA BIASHARA TANZANIA




**Source:** Barometa ya Biashara ya Afrika ya Benki ya Stanbic, Toleo la 5

Urahisi wa biashara unaweza kupishana kati ya 0 na 100 ambapo 0 inaonyesha ugumu mkubwa sana wakati wa kufanya biashara na nchi nyingine, 50 katikati na 100 inaonyesha kutokuwa na matatizo wakati wa kufanya biashara na nchi nyingine. Katika matokeo ya utafiti wa SB ATB ya Octoba 2025 alama za kielezo cha urahisi wa kufanya biashara Tanzania ziliongezeka kidogo hadi 48 kutoka mwezi Agosti, 2024. Hii ina maana kuwa biashara zilizopitiwa Tanzania ziliona rahisi kidogo kufanya biashara kulingana na mwezi Agosti,2024.

Asia ikawa ndiyo mshirika wa baishara aliyependwa zaidi Tanzania miongoni mwa biashara zilizofanyiwa utafiti huu. Hii ilichukua nafasi za nchi za Kiafrika ambazo zilionekana kuwa zilipendwa zaidi mwezi Agosti,2024.(angalia Mchoro) 23). Upendeleo kwa Asia ulionekana katika biashara zote ziliofanyiwa utafiti, biashara ndogo (38%), biashara kubwa (69%), na makampuni (43%). Hususani biashara ambazo zimepitiwa zinaonyesha ongezeko kubwa kutoka Agosti, 2024, wakati sehemu ya biashara ndogo zikieleza kuwa Asia kama mshirika pendwa zaidi kutokana na bei ndogo ya bidhaa zao (76%) aina nyingi ya bidhaa zinazopatikana (68%) na gharama za chini za uagizaji (43%) .

**Mchoro: Washirika** wa Biashara wanaopendwa




**Chanzo:** Barometa ya Biashara ya Afrika ya Benki ya Stanbic, Toleo la 5

Biashara ambazo zimepitiwa ziliona kufanya biashara na sehemu nyingine za dunia (ROW) kuwa rahisi zaidi.

Sehemu ya biashara zilizopitiwa ambazo zimeona ufanyaji biashara na sehemu nyingine za dunia rahisi sana au rahisi mno iliongezeka hadi 22% kulingana na 16% mwezi Agosti, 2024. Wakati huo sehemu nyingine za dunia kuwa vigumu au vigumu sana ilipungua kutoka 33% Agosti, 2024 hadi 27% katika utafiti huu. Ongezeko hili kwa kiasi limetokana na jitihada za biashara ya kimataifa za karibuni. Hususani China ilitekeleza sera ya kuondoa ushuru wa forodha kuanzia Desemba 1, 2024 na kuondoa ushuru wa forodha asilimia 100 kwa mauzo ya nje ya Tanzania. Sera ya kuondoa ushuru wa forodha kabisa ilipunguza vikwazo vya kufikia masoko kwa bidhaa za Tanzania zinazoingia kwenye masoko ya Kichina hivyo kufungua njia kwa viwango vikubwa vya mauzo ya nje.

Pia hii inasaidia kwa mauzo ya nje muhimu ya kilimo kama vile korosho na mkonge. Tanga kuzinduliwa kwa sera ya kuondoa ushuru wa forodha hadi mwezi Machi 2025, uagizaji wa China kutoka nchi zilizoendelea kidogo mno (LDCs') Afrika, ikiwemo Tanzania, uliongezeka kwa 15% kulingana na kipindi kama hicho mwaka uliopita, ikionyesha athari chanya mintarafu mafanikio ya mauzo ya nje.

Mabadiliko haya ya sera yanarejewa kwa kuona kwamba kufanya biashara na sehemu nyingine za duniani ni rahisi zaidi.( Angalia Mchoro 24). Zaidi ya hapo "European Union's (EU) Annual Action Programme 2025 for Tanzania" ilijumuisha hatua za kuongeza ushindani na uendelevu wa minyororo ya thamani ya kilimo kwa ongezeko la upatikanaji masoko wa Umoja wa Ulaya na uwekezaji unaokusudiwa kuimarisha upatikanaji masoko kwa bidhaa za kilimo teule.

**69%** **ya biashara kubwa ambazo zimepitiwa zimetaja Asia kama Kanda ya biashara pendwa.**

> "Kupitia Jukwaa la Msaada wa Pamoja (USP), tumeunganishwa na mfumo wa Ulaya, "Strategia Corto System," ambako bidhaa nyingi za kilimo kama alizeti, kahawa, chai na maparachichi zinakwenda Ulaya kupitia mpango wa USP."
>
> Mwakilishi kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) Forodha

**Mchoro 24:** Mitazamo ya Biashara kuhusu urahisi wa biashara na sehemu nyingine za dunia




**Chanzo:** Barometa ya Biashara ya Afrika ya Benki ya Stanbic,Toleo la 5

Biashara ambazo zimepitiwa zinaonekana kutojali kuhusu ufanyaji biashara na Afrika iliyobaki(ROA). Katika mawimbi yote matatu yaliyopita, urahisi na ugumu wa ufanyaji biashara na Afrika, ulishuka wakati kiwango cha kutojali kiliongezeka hadi 53% katika utafiti huu, kulinganisha na 28% Septemba 2022 (angalia Mchoro 25%). Sababu ambazo aghalabu hutajwa kwa kuona kufanya biashara na Afrika kuwa ngumu ni sera mbaya za biashara na nchi nyingine (24%) na miundombinu mibaya katika nchi nyingine (22%). Kinyume chake, wale ambao wameona kufanya biashara na Afrika iliyobaki kuwa rahisi aghalabu walitaja urahisi wa taratibu na ufanyaji biashara (30%), uhusiano mzuri wa kufanya biashara (28%) na bidhaa rahisi(20%).

**Mchoro 25:** Mitazamo ya ufanyaji biashara na Afrika iliyobaki




Chanzo: Barometa ya Biashara Afrika ya Benki ya Stanbic, Toleo la 5

Ufahamu wa "African Continental Free Trade Area" (AFCFTA) miongoni mwa biashara zilizopitiliwa haukubadilika. Sehemu ya biashara zilizopitiwa (298) ambayo inajua AFCFTA) haikubadilika kuanzia Agosti, 2024. Husussan zaidi hii ilisukumwa na tofauti katika maeneo yaliyopitiwa na utafiti. Sehemu ya biashara ambazo zimepitiwa ambazo zinaijua AFCFTA imeongezeka hadi 32% kulinganisha na 22% mwezi Agosti, 2024. Kinyume chake, uelewa miongoni mwa biashara kubwa na makampuni yaliyopitiwa zilishuka katika kipindi kama hicho (angalia Mchoro 26).

**Mchoro 26:** Ufahamu wa "African Continental Free Trade Area (1% ya biashara zilizopitiwa)




**Chanzo:** Barometa ya Biashara ya Afrika ya Benkiy a Stanbic, Toleo la 5

Huu ni ugunduzi mzuri ukichukulia matukio makubwa wawili mintarafu CFTA yaliyofanyika Tanzania mwaka 2025. Mnamo mwezi Juni, 2025 "The Africa Organisation for Standardisation" (ARSO) ulifanya Mkutano Mkuu wake wa 31 Zanzibar chini ya mada Uongezaji Kasi ya Biashara Nzuri na Haki Afrika chini ya "African Continental Free Trade Area ni Continental Regulatory Framework and Hamonised Standard" ikihudhuriwa na secretariat ya AFCFTA, mawaziri wa Tanzania, SME ya Tanzania, watengenezaji na wadau wakuu wa masoko. Tukio lilikuwa na lengo la kuona haja ya kukuza uwezo na ushindani wa wazalishaji, wafanyabiashara na SME's kushiriki katika minyororo ya thamani ya kikanda na kidunia na kupata masoko kikanda na kimataifa kwa kukidhi mahitaji ya viwango.

Zaidi ya hayo Mkutano wa Biashara na Uwekezaji wa Afrika 2025, ulifanyika Dar es Salaam ikizingatia "Tanzanias' Vision 2025", Agenda ya Umoja wa Afrika 2023 na AFCFTA. Tukio lilikusudiwa kuipanga upya Afrika ndani ya masoko ya dunia, kuimarisha biashara ndani ya Afrika, na kuelezea nafasi ya kimkakati ya Tanzania kama lango la Afrika Mashariki na Kusini.

Licha ya kutobadilika kwa uelewa, biashara zilizopitiwa zimezidi kutambua faida ya AFCFTA.

Faida kubwa tatu ambazo zimetajwa ni kuruhusiwa kwa hisa kubwa ya soko (31%) inayoruhusu ushindani mkubwa (28%) na urahisi wa upitishaji mizigo na huduma kuvuka mipaka (26%).(angalia Mchoro 27%). Ongezeko la biashara zilizopitiwa kutaja urahisi wa usafirishaji mizigo na huduma kuvuka mipaka lilisukumwa zaidi na biashara ndogo na makampuni yaliyofanyiwa utafiti. Husussan sehemu ya biashara zilizopitiwa zilitaja kuwa faida hii imeongoza sana hadi 24% kulinganisha na 12% mwezi August, 2024.

**53%** ya biashara zilizopitiwa zimeona ufanyaji biashara na Afrika iliyobaki kuwa sio rahisi wala mgumu.

**Mchoro: Faida** za Eneo Huru la Biashara la Afrika (% ya biashara zilizopitiwa)




> Hakika AFCFTA ni fursa kwa watengenezaji wa Tanzania, Soko lako linakua kwa sababu upeo wa soko unakuwa mkubwa zaidi. Kama utaona kama ni fursa utaifuatilia na kunufaika.
>
> Mwakilishi kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA)

# HITIMISHO

Mtazamo wa kiuchumi wa ndani wa Tanzania unabaki imara kwa kushikilia nafasi yake madhubuti katika mvuto wa kibiashara wa kanda. Uimara huu unaongezwa na kuchaguliwa tena kwa Rais Samia Suluhu Hassan mwezi Oktoba, 2025, jambo linaloashiria muendelezo wa sera na uimara kwa jumuia ya biashara. Nchi ilibaki na nafasi yake ya nne katika Barometa ya Biashara ya Afrika ya Benki ya Stanbic, ikisaidiwa na ukuaji imara wa GDP, uliokisiwa kuwa 5.8% mwisho wa 2025. Biashara zilizopitiwa zimeonyesha viwango vya imani vikisukumwa na matarajio ya ongezeko la uzalishaji. Ingawa kushuka kwa thamani ya fedha ilibaki kuwa changamoto, Benki Kuu ya Tanzania kwa mafanikio ilidhibiti mfumuko wa bei kwa wastani wa 3.4% na kutoa mazingira saidizi kwa shughuli na biashara zinazoendelea.

Kuimarika kwa uthabiti kwa msingi wa miundombinu ikisukumwa na miundombinu ya kiuchumi mikubwa na hatua madhubuti za kimkakati wa tabianchi vilikuza shughuli za biashara.

Kielezo cha msaada wa Serikali kiliongezeka kutoka 65 Mwezi Augasti, 2024 hadi 69 katika utafiti huu ikiakisi muendelezo wa uimarika mzuri wa namna ambavyo biashara zilizopitiwa zinaona wajibu wa Serikali katika kusaidia biashara. Uboreshaji huu kwa kiasi kikubwa unatokana kwa kukamilika kwa miradi ya kitaifa kama Reli ya Kisasa (SGR) na Kituo cha Kufua Umeme kwa Maji cha Julius Nyerere.

Zaidi, mkazo wa Serikali kwenye muungano wa kanda kupitia uondoaji wa vikwazo visivyo vya ushuru na utekelezaji wa mfumo wa kielektroni wa uondoshaji shehena umepunguza vikwazo vya kiutawala. Mageuzi haya yaliyokusudiwa pamoja na ushoroba wa biashara uliolengwa dhidi ya hali ya hewa vimeimarisha imani ya biashara katika miundombinu ya biashara miundombinu ya biashara ya nchi na mifumo ya kisasa. Taswira ya biashara inaelekezwa upya kwa muungano mkubwa na Asia na mienendo ya kikanda inayobadilika.

Kielezo cha uwazi wa biashara ya Tanzania kimeongezeka kikisukumwa kwa muongezeko wa uagizaji wa thamani kubwa kutoka China kusaidia miundombinu na miradi ya nishati mbadala. Wakati 81% ya biashara zilizopitiwa zinauza nje sehemu nyingine za Afrika, biashara na Afrika Mashariki ilikumbana na msuguano kufuatia masharti ya kibiashara magumu zaidi kwa makampuni ya kigeni yaliyoanzishwa Mwezi Julai, 2025 ambayo yalizuia wasiokuwa raia kufanya biashara rejareja, uwakala wa huduma za pesa kwa simu na ununuaji wa mazao shambani. Lakini wauza bidhaa nje wana imani zaidi kuhusu upatikanaji wa masoko ya dunia kwa vile Serikali inashawishi "AFCFTA Guided Trade Initiative" pia ikijitanua nje ya masoko ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Asia. Aidha mpango wa Utekelezaji wa Mwaka wa Umoja wa Ulaya pia uliongeza ushindani wa mnyororo wa kilimo wa Tanzania, na kutoa mbadala imara zaidi kwa masoko tete ya kikanda.



# II VIAMBATISHO

## Kiambatishi I: Barometa ya Biashara ya Afrika ya Benki ya Stanbic (SB ATB) Viwango vya Toleo la 5, 2025

Alama za Barometa ya Biashara ya Afrika ya Benki ya Stanbic (SB ATB) ni mkusanyiko wa alama za wingi wa Barometa ya Biashara ya Afrika ya Benki ya Stanbic (DB QTB) kwa miaka mitatu na Barometa ya Mapitio ya Biashara ya Benkiy a Stanbic. Nchi zinalinganishwa kati yao, yaani uwiano wa alama kati yao. Hii inapimwa katika kipimo cha 0-100. Zikipangwa katika kiwango hiki Msumbiji ina kielezo cha juu kabisa cha ufanyaji biashara wakati Zambia ina cha chini kabisa. Hii haina maana kuwa mtu hawezi kufanya biashara Zambia au Msumbiji ina kila kitu. Ina maana tu kuwa alama ya chini ni 0 na alama ya juu ni 100. Hivi ndivyo masoko hayo mawili yalivyokuwa.

Alama za SB ATB zilibaki sawa kwa Uganda, wakati ambapo nusu ya nchi ziliona alama zao zikiongezeka kutoka Agosti, 2024 (Angalia Jedwali 2)

Nchi ambazo zimedunisha viwango vyake kutoka Agosti, 2024:

- Nigeria (nafasi ya 5)
- **Tanzania (nafasi ya 4)**
- Uganda (nafasi ya 9)

**Nchi ambazo zimeongezeka katika viwango vyake kutoka Agosti,2024:**

- Angola (nafasi ya 10 hadi ya 8)
- Ghana (nafasi ya 7 hadi 6)
- Msumbiji ( nafasi ya 3 hadi ya 1)

**Nchi ambazo zimeshuka katika viwango vyake kuanzia Agosti, 2024:**

- Kenya(nafasi ya 6 hadi ya 7)
- Namibia (nafasi ya 2 hadi ya 3)
- Afika Kusini (nafasi ya 1 hadi ya 2)
- Zambia (nafasi ya 8 hadi ya 10)

**Jedwali 2:** Barometa ya Biashara ya Afrika ya Benki ya Stanbic (SB ATB) alama kwa nchi

| Barometa ya Biashara Afrika (ATB) | | | ATB Nafasi | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Aug '24 | Oct '25 | |
| Angola | 10 | 0 | 10 | 8 | ▲ |
| Ghana | 24 | 14 | 7 | 6 | ▲ |
| **Kenya** | 21 | 16 | 6 | 7 | ▼ |
| Msumbiji | 100 | 29 | 3 | 1 | ▲ |
| Namibia | 44 | 43 | 2 | 3 | ▼ |
| Nigeria | 30 | 19 | 5 | 5 | ● |
| Afrika Kusini | 90 | 100 | 1 | 2 | ▼ |
| Tanzania | 31 | 25 | 4 | 4 | ● |
| Uganda | 7 | 7 | 9 | 9 | ● |
| Zambia | 0 | 13 | 8 | 10 | ▼ |

**Chanzo:** Barometa ya Biashara ya Afrika ya Benki ya Benki ya Stanbic, Toleo la 5

**Maelezo: Alama zinaonyesha utendaji wa kila nchi kulingana na orodha ya nchi zote katika vipimo vilivyotumiwa.**

## **Kiambatisho 2:** Barometa ya wingi wa Biashara kwa miaka 3 ya Benki ya Stanbic (SB QTD) Viwango vya Nchi kwa Toleo la 5, 2025

Alama za SBTQ ziliongezeka kwa Ghana, Msumbiji na Nigeria ambapo alama za Angola zilibaki kama zilivyo. Kenya, Namibia, Afrika Kusini,Tanzania, Uganda na Zambia alama zake zilishuka kuanzia Agosti, 2024 (Angalia Mchoro 3)

**Nchi ambazo zilibaki na nafasi kuanzia Agosti 2024**

- Angola (nafasi ya 10)
- Nigeria (nafasi ya 4)
- **Tanzania (nafasi ya 7)**
- Uganda (nafasi ya 9)

**Nchi ambazo zimepanda katika nafasi zao kuanzia Agosti,2024:**

- Ghana (nafasi ya 8 hadi 5)
- Msumbiji (nafasi ya 3 hadi 1)

**Nchi ambazo zimeshuka katika nafasi zao kuanzia Agosti,2024:**

- Kenya (nafasi ya 5 hadi 6)
- Namibia (nafasi ya 2 hadi 3)
- Afrika Kusini (nafasi ya 1 hadi 2)
- Zambia (nafasi ya 6 hadi 8)

**Jedwali 3:** Barometa ya Wingi wa Biashara kwa miaka 3 ya Benki ya Stanbic (SB QTB) alama kwa kila nchi

| Barometa ya Wingi wa Biashara Alama za (QTB) | Alama (juu) | Alama (chini) | Nafasi ya QTB: Agosti '24 | Nafasi ya QTB: Oktoba '25 | |
|---|---|---|---|---|---|
| Angola | 0 | 0 | 10 | 10 | ● |
| Ghana | 23 | 20 | 8 | 5 | ▲ |
| Kenya | 19 | 22 | 5 | 6 | ▼ |
| Msumbiji | 100 | 37 | 3 | 1 | ▲ |
| Namibia | 36 | 45 | 2 | 3 | ▼ |
| Nigeria | 30 | 25 | 4 | 4 | ● |
| Afrika Kusini | 82 | 100 | 1 | 2 | ▼ |
| | 16 | 20 | 7 | 7 | ● |
| Tanzania | 9 | 11 | 9 | 9 | ● |
| Uganda | 9 | 21 | 6 | 8 | ▼ |

**Chanzo:** Barometa ya Biashara ya Afrika ya Benki ya Stanbic, Toleo la 5

**Kidokezo: Alama zinaonyesha utendaji wa kila nchi kulingana na vipimo vilivyoainishwa**

## Jedwali 3: Barometa ya Mapitio ya Biashara ya Benki ya Stanbic (SB STB) Viwango vya Nchi kwa Toleo la 5, 2025

**Barometa ya Biashara ya Mapitio ya Kampuni ya Benki ya Stanbic (SB STB) alama na nafasi kwa kila nchi ni wastani wa data yote iliyokusanywa kutoka mapitio ya utafiti wa msingi yaliyofanywa kwa biashara 2,218.**

**Alama za SBSTB hazijabadilika kwa Namibia, Tanzania na Zambia katika wimbi hili ambapo alama za nchi nyingine zilipanda.**

**Nchi ambazo zimeshikilia nafasi zao kuanzia Agosti 2024:**

- Msumbiji (Nafasi ya 9)
- Afrika Kusini (nafasi ya 4
- **Tanzania (nafasi ya 1)**
- Zambia (nafasi ya 10)

**Nchi ambazo zimepanda katika nafasi zao kuanzia Mei 2024:**

- Angola(Nafasi ya 3 hadi 2)
- Kenya (nafasi ya 7 hadi 5)
- Nigeria(nafasi ya 8 hadi 7)

**Nchi ambazo zimeshuka katika nafasi zao kuanzia Agosti, 2024:**

- Ghana ( nafasi ya 5 hadi 6)
- Namibia (nafasi ya 2 hadi 3)
- Uganda (nafasi ya 6 hadi 8)

**Jedwali: Barometa** ya Mapitio ya Biashara ya Benki ya Stanbic (SB STB) alama kwa nchi

| Barometa ya Mapitio ya Biashara Alama | | | Nafasi za STB | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Agosti '24 | Oktoba '25 | |
| Angola | 81 | 79 | 3 | 2 | ▲ |
| Ghana | 57 | 37 | 5 | 6 | ▼ |
| Kenya | 64 | 34 | 7 | 5 | ▲ |
| Msumbiji | 33 | 25 | 9 | 9 | ● |
| Namibia | 79 | 79 | 2 | 3 | ▼ |
| Nigeria | 55 | 31 | 8 | 7 | ▲ |
| Afrika Kusini | 78 | 44 | 4 | 4 | ● |
| Tanzania | 100 | 100 | 1 | 1 | ● |
| Uganda | 44 | 34 | 6 | 8 | ▼ |
| Zambia | 0 | 0 | 10 | 10 | ● |

**Chanzo:** Barometa ya Biashara Afrika ya Benki ya Stanbic, Toleo la 5

**Kidokezo: Alama zinaonyesha utendaji wa kila nchi kulingana na vipimo vilivyoainishwa.**

## Kiambatisho 4: Viashiria vya Uchumi Mkuu Vilivyochaguliwa kwa Tanzania

Kiambatisho hiki kimetengenezwa kuzingatia aina za viini vya Barometa ya Biashara Afrika ya Benki ya Stanbic: vinara wa uchumi mkuu, uwazi wa biashara na biashara ya nje, upatikanaji wa fedha na miundombinu. Hivi ni muhimu katika kutathmini mazingira ya biashara na matumizi ya nchi. Kwa kila kiini viashiria maalumu vimechaguliwa kuhesabu vitu vinavyochangia hali ya jumla ya kiuchumi. Data inaanzia mwaka 2020 kwa thamani zinazotabiriwa kwa mwaka 2025 na 2016, kutoa mtazamo wa muda kuhusu mielekeo na maelekezo yanayotarajiwa mbele.

Jedwali la 5: Mwonekano wa uchumimkuu wa Tanzania

| Aina za matini | Kiashiria | Kiasi | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024** | 2025** | 2026** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Vinara wa uchumi mkuu** | Pato la taifa kwa mtu | USD | 1 157 | 1 213 | 1 272 | 1 256 | 1 215 | 1 312 | 1 451 |
| | Pato la taifa | USD, Bilioni | 62.80 | 67.80 | 73.40 | 77.50 | 80.60 | 89.40 | 98.90 |
| | Kiwango Cha ukuaji halisi wa pato la taifa | % | 4.8 | 4.8 | 4.7 | 5.1 | 5.5 | 5.8 | 6.1 |
| | Kiwango cha mfumuko wa bei | % | 3.3 | 3.7 | 4.4 | 3.7 | 3.1 | 3.4 | 3.6 |
| | Uimara wa ubadilishaji wa fedha za kigeni kwa (USD/TZS) | TZS kwa USD | 2313.6 | 2303.8 | 2327.1 | 2435.5 | 2582.5 | 2544.6 | 2529.7 |
| | Kiwango cha punguzo cha BoT | % | 5.5 | 5 | 5 | 5 | 5.9 | 5.9 | 5.8 |
| | Akiba ya FX | Bilioni za USD | 4.7 | 6.4 | 5.2 | 5.5 | 5.7 | 6.7 | 7.7 |
| | Deni la ndani(% ya GDP) | % | 10.7 | 12.6 | 14.7 | 16.0 | 15.3 | 14.9 | 17.5 |
| | Deni la nje (% ya GDP) | % | 28.0 | 30.1 | 28.1 | 29.5 | 31.7 | 30.1 | 30.9 |
| **Uwazi wa biashara na biashara ya nje** | Biashara (Mauzo) ya nje na uagizaji kama% GDP) | % | 28.0 | 30.0 | 35.0 | 38.0 | 42.0 | Hakuna | Hakuna |
| | Biashara ya bidhaa | % of GDP | 21.9 | 23.2 | 27.8 | 26.6 | 29.3 | Hakuna | Hakuna |
| | Uwiano wa biashara | Bilioni za USD | -0.1 | -1.8 | -5.1 | -6 | -5.2 | -4.6 | -5.1 |
| | Akaunti ya hundi(%ya GDP) | % | -1.5 | -3.5 | -7.5 | -3.8 | -2.5 | -2.2 | -2.2 |
| | Mauzo ya nje ya bidhaa na huduma | Bilioni za USD | 8.8 | 10.0 | 11.6 | 14.0 | 16.0 | 17.6 | 17.8 |
| | Uagizaji wa bidhaa na huduma | Bilioni za USD | 8.9 | 19.9 | 16.7 | 16.1 | -16.9 | -17.9 | -18.9 |
| **Upatikanaji wa fedha** | Uundaji wa mtaji jumla (% ya GDP) | % | 12.4 | 13.0 | 15.2 | 16.4 | 16.8 | Hakuna | Hakuna |
| | Msaada kamili rasmi wa maendeleo uliopatikana | % | 38.8 | 39.7 | 41.1 | 41 | 40 | Hakuna | Hakuna |
| | Net official development assistance and official aid received | Bilioni za USD | 2.3 | 2.6 | 2.7 | 3.1 | Hakuna | Hakuna | |
| | Personal remittances received (% of GDP) | % | 0.5 | 0.8 | 0.9 | 1.0 | 1.0 | Hakuna | Hakuna |
| | FDI | Bilioni za USD | 0.9 | 1.2 | 1.4 | 1.6 | 1.7 | 1.8 | 2.2 |
| **Miundombinu** | Watu binafsi wanaotumia Intaneti (% ya idadi ya watu) | % | 18.0 | 19.0 | 22.0 | 29.0 | Hakuna | Hakuna | Hakuna |
| | Upatikanaji wa umeme( % ya watu wote) | % | 39.9 | 42.7 | 45.8 | 48.3 | Hakuna | Hakuna | Hakuna |
| | Matumizi ya simu za mkononi (kwa watu 100) | Uwiano | 84.0 | 86.0 | 93 | 105 | Hakuna | Hakuna | Hakuna |
| | Usafiri wa anga, mzigo | Tani milioni km | 1 | 4 | Hakuna | Hakuna | Hakuna | Hakuna | Hakuna |
| | Mfumo wote wa barabara (Barabara za lami na za mikononi) | Maelfu ya Kilometa | 9.8 | 11.2 | Hakuna | Hakuna | Hakuna | Hakuna | Hakuna |
| | Miundombinu ya reli | Jumla ya masafa-kuu | 564 | 637 | Hakuna | Hakuna | Hakuna | Hakuna | Hakuna |
| | Usafiri wa bandari na makontena | Maelfu ya TEU | 16.2 | 18.3 | Hakuna | Hakuna | Hakuna | Hakuna | Hakuna |

Chanzo: Benki ya Stanbic; 2025: Inapatikana hapa/ Benki ya Dunia; Inapatikana hapa. Umoja wa Mawasiliana ya Simu Duniani ( ITU): Ofisi ya Takrimu ya Taifa: Inapatikana hapa.

**Kidokezo: "Tija hasi inaonyesha kwamba nchi inaagiza tu ambapo tija chanya inaonyesha nchi inasafirishaji nje tu. Alama za data za mwaka 2025 na alama za data za mwaka 2026 zinakadiriwa. TEU Sawa na futi ishirini. Haipatikani ina maana kwamba data husika haikuwepo kutoka chanzo kilichoanishwa.**

**Kidokezo: Tarifa iliyokusanywa ni hadi Januari 2025 na makadirio yaweza kurekebishwa wakati wa uchapishaji.**.

## Kiambatanisho 5: Matokeo Muhimu ya Barometa ya Biashara ya Afrika ya Benki ya Stanbic, Toleo la 5, Mapitio ya Tanzania

Kiambatatisho kinawasilisha matokeo muhimu ya maswali makubwa yaliyoulizwa kuhusu biashara ya Tanzania kama sehemu ya nyongeza ya aiana ya Barometa ya Biashara ya Afrika ya Benki ya Stanbic. Matokeo yamepangwa kutokana na aina za matini: uimara wa uchumi mkuu, mwezi wa biashara na biashara ya nje , miundombinu, msaada wa serikali pamoja na tabia za kifedha za wafanyabiashara na upataji wao wa fedha. Sio maswali yote katika mapitio ya SB ATS yamewasilishwa hapa. Maswali yaliyopo yamechaguliwa na kuwa mafupi kwa uwasilishaji sahihi. Maswali kuhusu hali ya jumla ya biashara na wahusika binafsi au yale yanaiyohitaji majibu marefu yameachwa. Mtazamo huu unahakikisha kwamba matokeo yaliyoelezwa kwa kila katika Jedwali lifuatalo ni muhimu moja kwa moja na ya maana katika kutafsiri mienendo ya biashara katika muktadha wa Tanzania.

### Jedwali 6: Matokeo muhimu ya mapitio.

| | Swali | Majibu | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Uimara wa uchumi mkuu** | Ukifikiria faida ya biashara yako(kutoka 2020 hadi 2021), tafadhali onyesha kama faida yako iliongezeka, ilipungua au kubaki kama ilivyo | Imeongezeka | Imepungua | Imebaki vilevile | | Sijui | Amekataa | | | |
| | | Hakuna | Hakuna | Hakuna | | Hakuna | | | | |
| | Ukiangalia mbele kutoka 2024 hadi 2025), unategemea faida ya biashara kuongezeka, kupungua au kubaki kama ilivyo? | Imeongezeka | Imepungua | Imebaki vilevile | | Sijui | Hakuna | | | |
| | | 89% | 5% | 4% | | 2% | Amekataa | | | |
| | Ukiangalia mbele (kutoka 2025 hadi 2026) unategemea faida ya biashara kuongezeka, kupungua au kubaki kama ilivyo? | Imeongezeka | Imepungua | Imebaki vilevile | | Sijui | Hakuna | | | |
| | | 88% | 4% | 7% | | 1% | Amekataa | | | |
| | Tafadhali onyesha unavyohisi kuhusu utendaji wa uchumi kuhusiana na biashara katika miaka 3 ijayo? | Matumaini Makubwa | Matumaini makubwa | Katikati | Matumaini yapo kiasi | Hakuna matumaini kabisa | Hakuna | Sijui | | |
| | | 23% | 51% | 24% | 2% | 1% | Amekataa | Hakuna | | |
| **Miundombinu** | (Miundombinu ya Barabara)Ungepinga ubora wa mambo yafuatayo sokoni | Nzuri Mno | Nzuri sana | Nzuri | Sio mbaya | Mbaya | Usiitegeme/ tumia hii | Sijui | | |
| | | 20% | 46% | 25% | 3% | 6% | Hakuna | Hakuna | | |
| | (Usambazaji wa maji) Ungepimaje ubora wa mambo yafuatayo sokoni | Nzuri Mno | Nzuri sana | Nzuri | Sio mbaya | Mbaya | Usiitegeme/ tumia hii | Sijui | | |
| | | 22% | 51% | 18% | 5% | 3% | Hakuna | 1% | | |
| | (Mawasiliano ya simu) Ungepimaje ubora wa mambo yafuatayo sokoni? | Nzuri Mno | Nzuri sana | Nzuri | Sio mbaya | Mbaya | Usiitegeme/ tumia hii | Sijui | | |
| | | 28% | 53% | 13% | 4% | 1% | Hakuna | 1% | | |
| | (Bandari) Ungepimaje ubora wa mambo yafuatayo sokoni? | Nzuri Mno | Nzuri sana | Nzuri | Sio mbaya | Mbaya | Usiitegeme/ tumia hii | Sijui | | |
| | | 12% | 36% | 42% | 4% | 3% | Hakuna | 3% | | |
| | (Viwanja vya Ndege) Ungepimaje ubora wa mambo yafuatayo sokoni? | Nzuri Mno | Nzuri sana | Nzuri | Sio mbaya | Mbaya | Usiitegeme/ tumia hii | Sijui | | |
| | | 19% | 46% | 28% | 3% | 1% | Hakuna | 3% | | |
| | (Forodha na Udhibiti wa Biashara) Ungepimaje ubora wa mambo yafuatayo sokoni? | Nzuri Mno | Nzuri sana | Nzuri | Sio mbaya | Mbaya | Usiitegeme/ tumia hii | Sijui | | |
| | | 17% | 25% | 38% | 11% | 8% | Hakuna | 1% | | |
| | (Ugawaji wa Umeme) Ungepimaje ubora wa mambo yafuatayo sokoni? | Nzuri Mno | Nzuri sana | Nzuri | Sio mbaya | Mbaya | Usiitegeme/ tumia hii | Sijui | | |
| | | 24% | 48% | 21% | 5% | 2% | Hakuna | Hakuna | | |
| | (Miundombinu ya Reli) Ungepimaje ubora wa mambo yafuatayo sokoni? | Nzuri Mno | Nzuri sana | Nzuri | Sio mbaya | Mbaya | Usiitegeme/ tumia hii | Sijui | | |
| | | 17% | 47% | 27% | 4% | 3% | 1% | 2% | | |

| | Swali | Majibu | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Uwazi wa Biashara na Bishara ya nje | Vipi unaweza kuongeza kiwango cha uingizaji katika miaka miwili ijayo? | Inawezekana kabisa | Inawezekana | Isiwezekane au inawezekana | | Haiwezekani | Haiwezekani kabisa | | | |
| | | 23% | 67% | 10% | | Hakuna | Hakuna | | | |
| | Vipi unaweza kuongeza kiwango cha uingizaji katika miaka miwili ijayo? | Haiwezekani kabisa | Haiwezekani | Inawezekana au isiwezekane | | Inawezekana | Inawezekana sana | | | |
| | | 9% | 9% | 45% | | 23% | 14% | | | |
| | Kwa kiasi gani kodi kuhusiana na viwango pamoja na ushuru inaathiri ukuaji wa biashara yako? | Athari kubwa mno | Athari kubwa | Athari kiasi | | Athari ndogo | Hakuna Athari | | | |
| | | 10% | 19% | 54% | | 11% | 6% | | | |
| | Kwa kiasi gani kodi kuhusiana na ushuru na udhibiti wa biashara inaathiri ukuaji wa biashara yako | Athari kubwa mno | Athari kubwa | Athari kiasi | | Athari ndogo | Hakuna Athari | | | |
| | | 11% | 17% | 57% | | 9% | 6% | | | |
| | Vipi unaweza kuongeza kiasi cha usafirishaji nje katika miaka 2 ijayo? | Inawezekana kabisa | Inawezekana | Isiwezekane au inawezekana | | Haiwezekani | Haiwezekani kabisa | | | |
| | | 31% | 38% | 31% | | Hakuna | Hakuna | | | |
| | Vipi unaweza kupunguza kiasi cha usafirishaji nje katika miaka ijayo? | Haiwezekani kabisa | Haiwezekani | Inawezekana au isiwezekane | | Inawezekana | Inawezekana sana | | | |
| | | Hakuna | Hakuna | 71% | | Hakuna | 29% | | | |
| | Kwa kiasi gani kodi kuhusiana na usafirishaji nje Pamoja na ushuru, inaathiri ukuaji wa biashara yake | Athari kubwa mno | Athari kubwa | Athari kiasi | | Athari ndogo | Hakuna Athari | | | |
| | | 14% | 18% | 54% | | 9% | 6% | | | |
| | Kwa kiasi gani ushuru kuhusiana na usafirishaji nje na udhibiti wa biashara unaathiri ukuaji wa biashara yako? | Athari kubwa mno | Athari kubwa | Athari kiasi | | Athari ndogo | Hakuna Athari | | | |
| | | 12% | 16% | 53% | | 11% | 8% | | | |
| | Kwa miezi yako ungeamua ufanyaji biashra na sehemu nyingine za Afrika ni rahisi mno, rahisi sana, sio rahisi wala sio vigumu sana au vigumu mno | Rahisi mno | Rahisi sana | Sio rahisi wala sio ngumu | Sio rahisi | Sio rahisi kabisa | Sijui | Amekataa | | |
| | | 4% | 14% | 53% | 16% | 7% | 6% | Hakuna | | |
| | Kwa maoni yako ungesema kufanya biashara na dunia kote(nje ya Afrika) ni rahisi mno, rahisi sana, sio rahisi wala vigumu, vigumu sana au vigumu mno | Rahisi mno | Rahisi sana | Sio rahisi wala sio ngumu | Sio rahisi | Sio rahisi kabisa | Sijui | Amekataa | | |
| | | 6% | 15% | 44% | 19% | 8% | 7% | Hakuna | | |
| | Unajua Mkataba wa Biashara Huru wa Bara la Afrika | Ndio | | | Hapana | | | | | |
| | | 29% | | | 71% | | | | | |
| | Zipi faida kubwa tatu za AFCFTA kwenye biashara yako? | Hakuna Faida kabisa | Inasaidia usafirishaji wa bidhaa/ huduma mipakani | Inaruhusu soko kubwa zaidi kwa bidhaa/ huduma zangu | Inasaidia Ushindani mkubwa | Inakagua upatikanaji wa bidhaa na huduma nyingi | Inasaidia usafirishaji, mtaji na watu mipakani | Inasaidia uwekezaji mkubwa kwenye nchi zote | Inakuza maendeleo ya viwanda katika nchi zote | Ukuaji wa mfumo wa malipo katika kanda |
| | | 14% | 26% | 31% | 28% | 24% | 26% | 24% | 15% | 12% |
| Msaada wa Serikali | Tafadhali onyesha namna serikali yako inasaidia shughuli za kibiashara ya mpakani? | 5 - Inasaidia mno | 4 | 3 | 2 | 1 - Haisaidii kabisa | Amekataa | Sijui | | |
| | | 19% | 42% | 24% | 7% | 1% | 1% | 6% | | |

| | Swali | Majibu | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Tabia ya kifedha ya wafanyabiashara na Upatikanaji Fedha | Tafadhali onyesha namna ilivyo vigumu au rahisi kupata mkopo kutoka asasi za kifedha | Rahisi mno | 4 | 3 | 2 | 1 - Ngumu sana | Amekataa | Sjui | | |
| | | 23% | 28% | 28% | 12% | 7% | 2% | 1% | | |
| | Kwa nini unapenda kutumia fedha taslimu kwa bidhaa zako au huduma unapofanya biashara na wasambazaji wan chi nyingine | Gharama/ada ndogo zaidi | Inaruhusu mazungumzo | | Ujuzi mdogo katika njia zingine za malipo | | Urahisi wa kushughulikia | | Faragha | Nyingine |
| | | 50% | 62% | | 26% | | 55% | | 33% | Hakuna |
| | Changamoto gani, kama zipo, unapata unapofanya biashara na wasambazaji katika nchi nyingine | Wizi | Kupotea kwa Pesa/ Hatari za kiusalama | | Ubadilikaji wa kubadili viwango vya pesa | | Matamko ya ushuru wa forodha | Usumbufu - wa kubeba kiasi kikubwa cha pesa | | Nyingine |
| | | 31% | 79% | | 45% | | 29% | 52% | | Hakuna |
| | Faida au motisha gani ingekutia moyo kuhamia kabisa kwenye chaneli rasmi (kama kadi malipo ya kielektroni uhamishaji wa kimataifa, unapofanya biashara na wasambazaji wa nchi nyingine | Mda mchache wa kufanikisha miamala | Uhitaji wa nyaraka chache | Viwango vya ubadilishaji pesa vyenye ushindani | Uhakika wa usalama | Miamala iliyorekodiwa | Nyingine | | | |
| | | 40% | 36% | 43% | 90% | 43% | Hakuna | | | |
| | Unatoa masharti ya mkopo kwa wateja wako? | Ndio | | | Hapana | | | | | |
| | | 35% | | | 65% | | | | | |
| | Una masharti ya mkopo na wasambazaji wako? | Ndio | | | Hapana | | | | | |
| | | 30% | | | 70% | | | | | |

# KUHUSU UTAFITI

Barometa ya Biashara ya Afrika ya Benki ya Stanbic inatokana na vyanzo vyote vya utafiti wa msingi na wa pili. Hili ni Toleo la 5 la SB ATB. Matoleo ya 1,2,3 na 4 yalitolewa mwezi Juni, 2022, Novemba, 2022, Septemba, 2023 na Agosti, 2024 mtawalia. Ukusanyaji wa data (ya msingi na ya pili) kwa Toleo la 5 ulifanyika kati ya Septemba na Oktoba, 2025 katika nchi zote 10 zenye maslahi.

Sehemu ya utafiti wa msingi inajumuisha utawala na uchambuzi (yaani mapitio ya sampuli za biashara katika nchi zenye maslahi) na mahojiano ya kina na wadau. Sampuli imepangwa kwa ukubwa (ndogo, kubwa na shirika/kampuni) kanda na kiwanda. Jumla ya biashara 2218 zilifanyiwa mapitio na mahojiano ya kina yalifanywa katika nchi zote 10 katika Toleo la 5.

**INchini Tanzania biashara 190 zilipitiwa 47% ya hizo ziko Dar es Salaam, 20% ziko Mwanza, 13% Arusha, 9% Mbeya na 11% Moshi. Mgawanyiko wa biashara zilizopitiwa Tanzania kwa kila sehemu ulikuwa kama ifuatavyo:**

- 68% zilikuwa biashara ndogo
- 16% zilikuwa biashara kubwa
- 16% yalikuwa mashirika

Katika muktadha wa SB ATB, biashara ndogo zinatafsiriwa kuwa ni zile zenye mauzo ya zaidi ya TZS Bilionii 92..

**Mgawanyiko wa biashara zilizopitiwa Tanzania kwa kila kiwanda ni kama ifuatavyol:**

Jedwali la 7: Mgawanyiko wa biashara zilizopitiwa kwa kiwanda

| Kiwanda | % | Kiwanda | % |
|---|---|---|---|
| Ujenzi | 16% | Elimu | 3 |
| Biashara ya jumla na rejareja, utengenezaji wa magari na pikipiki | 13% | Utawala wa umma na ulinzi | 3 |
| Usafirishaji na uhifadhi | 11 | Umeme, gesi, stimu na viyoyozi | 3 |
| Utengenezaji | 6 | Sanaa, burudani na mapumziko | 2 |
| Uchimbaji madini na mawe (pamoja na mafuta na gesi) | 6 | Shughuli za huduma nyingine | 2 |
| Upangishaji na shughuli za huduma ya chakula | 5 | Shughuli za mali isiyohamishika | 2 |
| Shughuli za kifedha na bima | 5 | Usambazaji maji, maji taka, chakula usimamiaji taka na shughuli za ukarabati | 1 |
| Afya ya binadamu na za kazi za kijamii | 5 | Shughuli za kaya kama waajiri; bima bidhaa zisizo tofautishwa na shughuli za utoaji huduma za kaya kwa matumizi binafsi | 1 |
| Taarifa na mawasiliano | 3 | Shughuli za kiweledi, Kisayansi na Kiufundi | 0 |
| Utawala na shughuli za kusaidia huduma | 3 | Shughuli za mashirika | 0 |

**Mgao wa biashara zilizopitiwa kwa kigezo cha wafanyakazi ulikuwa kama ifuatavyo:**

- 26% walikuwa na wafanyakazi chini ya 5
- 36% walikuwa na wafanyakazi 5-10
- 15% walikuwa na wafanyakazi 11-20
- 12% walikuwa na wafanyakazi 21-50
- 6% walikuwa na wafanyakazi 51-1000
- 4% walikuwa na wafanyakazi 101- 1000
- 1% walikuwa na wafanyakazi 1000-5000

**Kuhusiana na tabia za wahusika kwenye biasahara 63% walikuwa wanaume na 37% walikuwa wanawake. Mgao kwa vyeo vya kazi ni kama ifuatavyo::**

- 32% walikuwa wahasibu wakuu
- 25% walikuwa mameneja wakuu
- 22% walikuwa wenye mali, washiriki wa wenyemali au washiriki wenza
- 10% walikuwa wakuu wa Idara
- 4% walikuwa wakurugenzi wakuu
- 4% walikuwa maafisa wa fedha wakuu
- 2% walikuwa wakurugenzi watendaji
- 1% walikuwa wahazini
- 1% walikuwa wakurugenzi wakuu
- 1% walikuwa wenyeviti

Taarifa zaidi kwa mikoa, sehemu za biashara, watumishi wa viwanda miaka ya kampuni, mifumo ya uamuzi wa kimkakati ya makampuni Pamoja na tabia za wahusika binafsi (jinsia, cheo na kazi nk) zinapatikana inapoombwa.

Kulikuwa na mahojiano ya kina matatu yaliyofanywa Tanzania kama sehemu ya Toleo la 5. Mahojiano yalifanywa na wawakilishi kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania na Wizara ya Fedha na Mipango. Mahojiano haya yananukuliwa katika Ripoti hii kuwa muhimu.

Mapitio na mahojiano ya kina yalifanywa kwa siri.

Sehemu ya utafiti wa pili inahusu ukusanyaji na uchambuzi wa data ya wingi. Data hii kimsingi inakusanywa kutoka vyanzo vya Benki ya Dunia ingawa data ya ziada inapatikana kutoka Shirika la Fedha Duniani (IMF),Kituo cha Biashara cha Kimataifa na Benki Kuu za nchi mbalimbali.

Maelezo ya kina kuhusu namna ambayo alama za Barometa ya Biashara ya Afrika ya Benki ya Stanbic kwa kila nchi zinavyokokotolewa na nafasi zinazotokana kwa kila nchi zinapatikana zikitakiwa.

Utafiti ulitayarishwa na Standard Bank Business and Commercial. Kwa maswali yoyote au mahitaji ya taarifa kuhusu Ripoti hii tafadhali wasiliana na **tradebarometer@standardsbg.com**.

# KATAO

Ripoti hii ina utafiti huru wa The Standard Bank of South Africa Limited na wasambazaji wake wengine.

Ripoti hii ni kwa ajili ya taarifa ya jumla kwa umma. Mawazo na maoni yaliyokuwa katika ripoti hii ni kwa ajili ya taarifa tu sio lazima yaakisi sera rasmi au msimamo wa Standard Bank of South Afrika Limited na/au mshirika wao yoyote, Kampuni tanzu na kampuni mama (Standard Bank Group). Ripoti ilitayarsishwa na Standard Group kwa mujibu wa tarehe iliyotajwa na inaweza kurekebishwa bila taarifa ya awali. Maoni yaliyoelezwa ni maoni yetu ya sasa kwa mujibu wa data inayoonyeshwa kwenye Ripoti hii tu. Ripoti hii inatokana na taarifa ambayo tunaona ni ya kuaminika, lakini Standard Bank Group, haihakikishi wala kuwasilisha (kwa uwazi au hisia) kuwa ni sahihi, imekamilika, haipotoshi au kamilifu kwa madhumuni yaliyokusudiwa au kwamba haina makosa au upungufu Standard Bank Group na wafanhyakazi wake, mawakala na wawakilishi wake hawakubali dhima kwa kosa lolote, hasara au madai kutokana na matumizi ya taarifa yoyote iliyowasilishwa katika Ripoti hii na isitegemewe kama ilivyo.

Taarifa inayotolewa katika Ripoti hii haitoi ushauri na isitegemewe kama ushauri huru wa kiweledi, wa aina yoyote. Kabla ya kutumia ushauri wowote au mapendekezo katika Ripoti huu wapokeaji watafakari iwapo inafaa kwa mazingira yao maalumu na ikibidi watafute ushauri wa kiweledi.

Haki miliki 2026. Haki zote zimehifadhiwa. Ripoti hii au sehemu yake yoyote isiohapishwe, kuuzwa, kusambazwa, kuhaririwa, kurekebishwa, kutolewa upya au kutunzwa kwa madhumuni yoyote bila idhini ya maandishi ya The Standard Bank of South Afrika Limited.

